# BUNGE LA TANZANIA

# MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

## Kikao cha Saba – Tarehe 6 Septemba, 2023

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza maswali Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa Nyongo.

Na. 93

### Ujenzi wa Jengo Jipya la *X–Ray* Hosptali ya Wilaya Maswa

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO** aliuliza: -

Je, lini jengo jipya la *X-Ray* litajengwa katika Hospitali ya Wilaya ya Maswa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, Mbunge wa Jimbo la Maswa Mashariki kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia fursa ya mikopo inayotolewa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya *(NHIF)* inakamilisha taratibu za kupata mkopo wa shilingi milioni 190, kwa ajili ya ujenzi wa jengo la *X–Ray* katika Hospital ya Wilaya ya Maswa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kutokana na uchakavu wa baadhi ya majengo Serikali katika mwaka wa fedha 2023/2024 imetenga kiasi cha shilingi milioni 900, kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa majengo katika Hospitali ya Wilaya ya Maswa. Ahsante.

**NAIBU SPIKA*:*** Mheshimiwa Nyongo.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ni kwamba mkopo unaotolewa na *NHIF* ni wa shilingi milioni 200 na utaifanya hospitali yetu kulipa kiasi cha shilingi milioni 6,500,092 kwa mwezi, katika miezi 36, na itakuwa imelipa jumla ya shilingi milioni 237, pamoja na riba ya asilimia 11.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haioni nia njema ya Wilaya ya Maswa ya kukopa *NHIF* kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la *X–Ray* ili Serikali itoe fedha ambayo si mkopo kwa ajili ya ujenzi wa jengo hilo la *X–Ray* na wananchi wapate huduma?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ni lini Serikali vilevile itajenga Kituo cha Afya cha Kata ya Sangamwalugesha katika Kijiji cha Sangamwalugesha?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Nyongo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa miundombinu ya huduma za afya inatumia fedha za Serikali Kuu na fedha zinazotokana na makusanyo ya ndani, zikiwemo fedha za uchangiaji wa huduma za afya lakini pia na za Mfuko wa Bima ya Afya ya Taifa *(NHIF)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niwapongeze sana Halmashauri ya Maswa na nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge; kwa sababu yeye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii na amekuwa mfano mzuri kuonesha tunaweza tukatumia fursa za mikopo ya NHIF, tukaboresha miundombinu na hatimaye tukatoa huduma bora zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuhakikishie pamoja na kwamba tutakatwa shilingi milioni 6,500,000, bado watakuwa na uwezo wa kuendelea kujiendesha. Pia, jengo litakalojengwa litaongeza mapato ya Hospitali yetu hii ya Maswa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili kuhusiana na hiki kituo cha afya, naomba tulipokee tukafanyie tathmini, tuone kama kinafiti kwenye vituo vya afya vya kimkakati ili tuweze kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho cha afya. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Almas.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mahitaji ya jengo la X–Ray katika Wilaya ya Maswa, linafanana kabisa na Kituo cha Afya cha Upuge. Kuna mitambo pale kwa miaka mitano ipo kwenye mabox, *X–Ray* Mashine na *Ultrasound*. Lini Serikali itajenga jengo? Kwa sababu mitambo hii itaoza, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua fursa hii kwanza kumuelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri hii kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI; kwamba Serikali ilishapeleka mashine ya *X–Ray*, ilishapeleka *Ultrasound,* na wao kupitia mapato ya ndani wana uwezo wa kujenga jengo la *X–Ray* na *Ultrasound* ili wananchi waanze kupata huduma hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wajibu wao, na nitoe wito, kwamba wanatakiwa kuweka kwenye bajeti haraka iwezekanavyo, na ikiwezekana kwenye mapitio ya bajeti mwezi Desemba wananchi waanze kupata huduma za *X-Ray* na *Ultrasound*. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Janeth Massaburi.

Na. 94

**Ujenzi wa barabara za Dar es Salaam kwa Mfumo wa *EPC+F***

**MHE. JANETH M. MASSABURI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga barabara za mitaa za Mkoa wa Dar es Salaam kwa mfumo wa *EPC+F* kwa vile Mradi wa *DMDP* haukidhi haja?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Janeth Maurice Massaburi, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na ukamilishaji wa maandalizi ya Mradi wa *DMDP* Awamu ya Pili. Tayari wataalam washauri watatu wanaendelea na kazi ya usanifu ambapo mkataba wa kazi hiyo utafanyika kwa muda wa miezi sita kuanzia Tarehe 30 Mei, 2023. Mara tu usanifu utakapokamilika, taratibu za ununuzi wa kuwapata wakandarasi zitaanza kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, *EPC+F* ni mfumo wa ujenzi wa kimkataba ambapo mkandarasi anafanya usanifu, ununuzi, ujenzi na kugharamia kazi za ujenzi *(engineering design, procurement, construction and financing)*. Serikali kupitia *TARURA* bado haijaanza kutekeleza mfumo huu. Serikali inapokea ushauri na itapitia na kuufanyia kazi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Massaburi.

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Kwanza nichukue fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya katika kuendeleza miundombinu ya barabara hususan barabara ya *ring road,* Mkoa wa Dodoma. Kazi inaenda kwa kasi sana. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali namba moja; je, Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara ya mzunguko *(ring road)* katika Mkoa wa Dar es Salaam? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Serikali ina mpango gani wa dharura kutengeneza barabara ambayo iko pembezoni mwa reli, kuanzia maeneo ya *Machinga Complex* (jengo la Mheshimiwa Naibu Spika) kupitia Buguruni, Majumba Sita mpaka Ukonga na barabara inayotoka maeneo ya Mabibo Jeshini kupitia Barabara ya *TASAF* – Kimanga; je ni lini Serikali itajenga barabara hizo kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Massaburi, swali lako haliendani na swali la msingi. Linahitaji takwimu na Waziri kujiandaa. Kwa sababu, wewe umeuliza masuala ya *EPC+F*, sasa umekuja kwenye ujenzi wa *TARURA* tena. Nafikiri swali lako ni la msingi lakini lilete katika utaratibu wa kawaida.

Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mbarouk Juma Khatib.

Na. 95

**Hitaji la Kituo cha Polisi eneo la Bandari ya Mizigo – Zanzibar**

**MHE. MBAROUK JUMA KHATIBU** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kujenga Kituo cha Polisi katika eneo ambalo linajengwa Bandari Kuu ya mizigo Zanzibar?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbarouk Juma Khatibu, Mbunge wa Jimbo la Bumbwini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Bandari ambayo imejenga bandari ya mizigo eneo la Manga Pwani – Zanzibar

imetenga eneo na imeandaa michoro kwa ajili ya kujenga ofisi zitakazotumiwa na vyombo vya ulinzi na usalama kikiwemo kituo cha polisi, ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbarouk.

**MHE. MBAROUK JUMA KHATIBU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

(a) Je, hatuoni kuna haja ya kuharakisha ujenzi huu kutokana na uhalifu ambao unajitokeza?

(b) Je, Serikali haioni haja ya kuongeza nguvu ya askari na gari kwa ajili ya doria? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, najibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Khatibu, Mbunge wa Jimbo la Bumbwini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kumpongeza sana kwa kazi nzuri anayoifanya; lakini kikubwa nimwambie tu kwamba kuna haja ya kufanya haraka ya kituo hiki ipo na tayari Jeshi la Polisi kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi tumeshawasiliana na wenzetu wa Mamlaka ya Bandari – Zanzibar ili ikiwezekana haraka waweze kuanza ujenzi wa kituo hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaambie tu siyo kituo hiki, pale bandarini ni lazima pale pawe na watu wa uhamiaji, pawe na ofisi za *fire* na hicho kituo cha polisi ili lengo na madhumuni ni huduma za ulinzi na usalama katika eneo lile zipatikane.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, haja ya kuongeza askari ipo. Nimwambie tu Mheshimiwa awe na subira kidogo kwa sababu,

vijana wetu bado wapo kwenye mafunzo. Juzi tu Jeshi la Polisi walitangaza nafasi nyingine ili lengo na madhumuni tuongeze nguvu ya ulinzi na usalama katika maeneo yetu yote ya Tanzania, ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Mnzava.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Kata ya Isalamagazi ambayo ndiyo Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga kuna kituo cha polisi ambacho kimejengwa enzi za mkoloni.

Je, ni lini Serilkali itajenga kituo hicho? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali inatambua uchakavu wa baadhi ya vituo vya polisi na hata baadhi ya makazi ya Askari Polisi. Ndiyo maana Serikali tumo kwenye mbio ya kuhakikisha tunatafuta fedha ili tujenge vituo vya kisasa zaidi na viweze kutoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwambie tu Mheshimiwa kwamba Serikali tutakapopata fedha tutahakikisha kituo chake tunakipa kipaumbele ili wananchi waweze kupata huduma za ulinzi na usalama. Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Esther Matiko, kwa niaba ya Mheshimiwa Tendega.

Na. 96

**Watanzania walioandikishwa na kupatiwa Vitambulisho vya Taifa**

**MHE. GRACE V. TENDEGA K.n.y. MHE. ESTHER N. MATIKO** aliuliza:-

Je, ni asilimia ngapi ya Watanzania wameandikishwa na kupatiwa Vitambulisho vya Taifa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Tarehe 31 Julai, 2023, jumla ya Watanzania 11,242,736 wamepewa vitambulisho, sawa na asilimia 55 ya lengo la kuwapatia wananchi 20,294,910 wanaostahili kupewa. Mpango wa Serikali ni kuwagawia vitambulisho Watanzania waliobaki ifikapo Machi, 2024, ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tendega.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninaomba sasa niulize maswali mawili ya nyongeza.

a) Je, ni kwa nini Serikali inachukua muda mrefu kutoa vitambulisho kwa Watanzania, hamuoni kwamba mnawakosesha fursa mbalimbali ambapo kitambulisho ndiyo takwa la fursa hizo?

b) Je, ni lini Serikali itaoanisha data zote za msingi ili ziweze kusomeka kwenye kitambulisho hicho cha *NIDA*?

**NAIBU SPIKA**: Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa maswali haya mawili ya nyongeza. Naomba kutoa majibu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Matiko, amekuwa mara kadhaa akifuatilia kuona namna ambavyo Watanzania wanaweza kupata vitambulisho ili kuweza kupata huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haijachukua muda mrefu sana kutoa vitambulisho kwa watu; na kama imechukua basi tulikuwa tuna changamoto. Changamoto ya kwanza tulikuwa na upungufu wa mashine za kisasa ambazo zilikuwa zinatoa vitambulisho kwa *speed* kubwa. Niwaambie wananchi na Watanzania; sasa tumeshapata mashine bora za kisasa na tunakwenda kuhakikisha Watanzania wote wanapata vitambulisho ili waweze kupata huduma, kwa sababu tunatambua sasa hivi kila kitu ni kitambulisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingine. ninawomba Watanzania wote, wakamilishe taratibu ili tuweze kupata vitambulisho. Kuna watu wanashindwa kutoa baadhi ya *particulars* muhimu za kutengenezewa vitambulisho. Inakuwa ngumu kwetu kuweza kuwakamilishia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona kwamba tunavyo vitambulisho vingi. Tuone namna ya kuviunganisha vitambulisho hivyo ili kiwe kimoja. Maana yake hicho hicho kiwe na uwezo wa kutumika benki, kwenye *passport* unaweza ukawa unakitumia kama *NIDA* au kitambulisho kingine. Tuko mbioni kuona namna ambavyo Serikali itapunguza changamoto hiyo, ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Mhata, *sorry* Mheshimiwa Nyangidu.

Na. 97

**Hitaji la mabwawa ya mifugo – Kishapu**

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO** aliuliza: -

Je, lini mabwawa ya mifugo yatachimbwa Kata za Lagama, Masanga Mwamalasa, Ngofila, Bunambiyu, Mwasubi na Somagedi – Kishapu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo, Mbunge wa Kishapu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua changamoto ya upatikanaji wa maji kwa ajili ya mifugo katika maeneo mbalimbali hapa nchini ikiwemo katika Jimbo la Kishapu. Kazi ya ujenzi wa mabwawa hufanyika kwa hatua kuu tatu ambazo ni; kutafuta chanzo cha maji *(water source)*, kufanya usanifu na kuanza ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa kutambua changamoto ya upatikanaji wa maji katika jimbo la Kishapu hususani katika kata alizozitaja Mheshimiwa Mbunge, naomba kutoa wito kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu kwa kushirikiana na wataalam wa Wakala ya Huduma na Usafi wa Maji Vijijini *(RUWASA)*, kuanza kazi ya kutafuta chanzo cha maji katika maeneo husika, kuandaa michoro *(design)* na mchanganuo wa gharama *(BOQ)* ili kuweza kupewa kipaumbele kwenye mpango na bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa wito kwa wafugaji na wadau wengine, kuwekeza kwenye ujenzi wa miundombinu ya

maji ya mifugo ili kusaidia kupunguza changamoto ya maji kwa ajili ya mifugo hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Butondo.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali yaliyotolewa. Ninaomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo jitihada kubwa ambazo zilishafanywa huko nyuma na wananchi kupitia utaratibu wa Vijiji vya Ujamaa na nguvu za wananchi kuhakikisha kwamba wanachimba mabwawa katika kipindi cha nyuma. Hapa miaka ya 90 mpaka 2000, Serikali iliweza kuchiba baadhi ya mabwawa, lakini mabwawa yale ni kama yalitelekezwa na baadaye yakawa yameharibika. Kuna uhitaji ama umuhimu wa kuyafufua yale mabwawa ambayo yalichibwa nyakati hizo, kabla ya kuweka mkakati wa muda mrefu ule wa kujenga mabwawa haya.

Je, ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha mabwawa yaliyopo katika maeneo hayo yanafufuliwa kwanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza natumia nafasi hii kumpongeza sana Mbunge wa Kishapu, Mheshimiwa Boniphace Nyangindu, kwa kazi kubwa anayoifanya ya kufatilia namna ambavyo wafugaji wake wanatakiwa wawe na maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyouliza swali lake la msingi, ni kweli kwamba Serikali ipo na mipango mingi ya kufufua mabwawa yote yaliyokufa. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, baada ya Bunge hili tutatuma wataalam kuja kufanya tathmini katika jimbo lake. Tujue tathmini hiyo, mabwawa yako mangapi na

yanahitaji nini ili Wizara kamaSerikali Wizara iweze kutuma namna ya kuyafufua haya mabwawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua mabwawa ambayo yanahitaji kufufuliwa na Serikali yapo maeneo mengi. Serikali tunamuahidi Mheshimiwa Mbunge Serikali imejipanga vizuri. Tukishapata kujua gharama za shilingi ngapi inatakiwa kwenda kuyafufua hayo mabwawa tupo tayari kwenda kuyafufua mabwawa hayo kwenye Jimbo la Kishapu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mhata.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na migogoro mikubwa kati ya wafugaji na wakulima. Ndani ya Jimbo langu la Nanyumbu wakulima wa Kata ya Lumesule wana mgogoro mkubwa na wafugaji wa eneo hilo. Hii imepelekea kuhatarisha hata maisha yao. Hivi ninavyozungumza wakulima wako katika hali mbaya sana ya usalama kati yao na wafugaji.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri upo tayari mara baada ya kuahirishwa Bunge letu kesho kutwa, mimi na wewe tukafuatana tukaenda kwenye Kata husika kutatua mgogoro uliopo kati ya wakulima na wafugaji? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge anataka kujua kama Wizara iko tayari kuambatana naye baada ya Bunge hili. Wizara iko tayari kuandamana na Mheshimiwa Mbunge. Tuko tayari kwenda kuona mgogoro huu na kuutafutia ufumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla Wizara haijaenda kutafuta ufumbuzi wa mgogoro huu Serikali hii ni kubwa, wapo viongozi ambao wanapaswa kuanza kuhangaika na migogoro hii kabla Wizara haijafika huko. Yupo Mheshimiwa *DC*, nitoe wito sana, Mheshimiwa *DC* na wataalam wote waliopo huko wa Mifugo na Kilimo kwenda kutatua mgogoro huu kabla Wizara haijafika huko kutafuta ufumbuzi wa kudumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ina Wataalam wa Kilimo na Mifugo, ina Mheshimiwa *DC* ambaye ni Kamisaa wao. Tunaomba kabla Wizara haijafika huko nitoe wito kwa wakuu wote waende kutatua mgogoro huu kabla hatujafika huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Husna Sekiboko.

Na. 98

**Kutambua gunia kama kifungashio au kipimo**

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO** aliuliza: -

Je, Serikali inatambua gunia kuwa kipimo au kifungashio kwa mujibu wa Sheria?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Vipimo, *The Weights and Measures Act (Amendment) Order, G.N. No. 725 of 2018*, jedwali la 10 chini ya kifungu cha 2(b) cha Jedwali hilo ambacho kinasema mazao ya mashambani yatafungashwa kwa uzito usiozidi kilogramu 100. Pamoja na kuelekeza wauzaji au wanunuzi wa mazao kutumia mizani, Serikali haitambui gunia kuwa kipimo bali ni kifungashio.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo nitoe wito kwa wadau wote kuepuka matumizi ya gunia kama kipimo kwani kwa kufanya hivyo ni kukiuka Sheria ya Vipimo, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Husna.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwanza nashukuru sana kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Swali la kwanza; kwa kuwa sasa Serikali imekiri kwamba gunia sio kipimo ni kifungashio. Je, Serikali iko tayari sasa kutoa waraka na kupeleka kwa Wakala wa Vipimo na Halmashauri zote nchini kuzuia tabia ya kushusha magunia katikati ya safari na kuanza kuyapima barabarani?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kuna mazao kama mbogamboga, matunda na viazi yamekuwa yakipimwa kwenye soko kwa kilo, lakini shambani yamekuwa yakipimwa kwa magunia. Je, Serikali iko tayari sasa kutoa kipimo cha awali kwa ajili ya mazao ya aina hiyo, namna ambavyo yanaweza kupimwa yakiwa shambani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa kutoa *concern* ya wenzetu wa Halmashauri na Wakala wa Vipimo kukagua magunia au mazao yanayopita katika sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tumeshasema kwamba, kama wananchi wameuza kwa vipimo na kukawa na uthibitisho wa kwamba mazao yale kama *either* yamefungashwa katika magunia au katika vifungashio (vibebesheo) vyovyote kama vina uthibitisho kwamba yameuzwa kwa vipimo, wale wanaokagua aidha Wakala wa Vipimo au Halmashauri watumie zile risiti au vielelezo vyovyote *(evidence)* ili ziwe ni sehemu ya kupunguza usumbufu kwa wananchi, wakulima au wafanyabiashara wanaposafirisha mazao badala ya kupima kila gunia kwenye maeneo ya ukaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuhusiana na suala la mbogamboga. Haya bado ni maelekezo, katika mazao yote kwamba, katika maeneo mengi tunahamasisha wakulima wajiunge katika Vyama vya Msingi au wauzie kwenye masoko ambako kule sisi tumeshaelekeza Wakala wa Vipimo wapeleke mizani ili itumike kupima uzito wa bidhaa inayouzwa badala ya kutumika vifungashio vya namna yoyote ile ambavyo havitumii vipimo sahihi, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mheshimiwa Janeth Mahawanga.

Na. 99

**Majukwaa ya kuwezesha wanawake kiuchumi kuleta tija**

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA** aliuliza:-

Je, nini mpango wa kuhakikisha Majukwaa ya Kuwezesha Wanawake Kiuchumi yanaleta tija kwenye mikopo ya asilimia 10 ya Halmashauri?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi yameleta tija kwenye asilimia 10 ya Halmashauri ya kuwezesha kuunda vikundi vya kiuchumi ambavyo hukutanisha wanawake katika ngazi zote za jamii ili kujadili fursa, changamoto na jinsi ya kushiriki katika shughuli za kiuchumi hususan biashara, kilimo, madini, ujenzi, uchukuzi, usindikaji wa maliasili na mazao ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali katika jamii, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Janeth Elias.

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali lakini, nina maswali madogo mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; Vikundi vingi vya Majukwaa bado havina uelewa wa pamoja wa lengo mahsusi la uanzishaji wa majukwaa haya. Sasa nini kauli ya Serikali kuhusu hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; ni utaratibu upi unatumika kahakikisha waratibu wa majukwaa haya wanashuka kutoa elimu ya mwongozo wa uratibu wa majukwaa haya katika ngazi ya kata na mitaa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tunaendelea kutoa mafunzo kwa lengo la kukuza uelewa kwa majukwaa haya ya kuendeleza uchumi kwa ajili ya wanawake. Napenda kutoa rai kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii, kuhakikisha kwamba wanatoa mafunzo kwa lengo la

kuwaelewesha wananchi ni nini cha kufanya katika majukwaa haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Wizara yangu inafuatilia na kufanya tathmini mbalimbali katika vikundi vyote vya majukwaa ya wanawake kiuchumi na kuhakikisha kwamba tunawatembelea kila baada ya robo ya mwaka wa fedha kuhakikisha vikundi vile vinafanya kazi vizuri na kuhakikisha wanafuata sera, sheria, kanuni na miongozo yote ambayo tumeipanga, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Katani Katani.

Na. 100

**Barabara ya Mtwara – Nanyamba – Tandahimba – Newala – Masasi**

**MHE. KATANI A. KATANI** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa kiwango cha lami wa Barabara ya Mtwara – Nanyamba – Tandahimba – Newala hadi Masasi utaanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile ni mara yangu ya kwanza toka Mheshimiwa Rais wetu mpendwa, Dkt. Samia Suluhu Hassan ameniteua kumsaidia katika jukumu la Waziri wa Ujenzi, kwa kibali chako naomba kwanza nianze kwa kutoa shukrani kwa Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuniamini. Namwahidi Mheshimiwa Rais sitomwangusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, Mhandisi Godfrey Kasekenya, kwa kuendelea kuaminiwa na Mheshimiwa Rais. Namwahidi Mheshimiwa

Rais, tutafanya kazi kwa bidii tutapambana na kudhibiti rushwa hasa kwenye maeneo ya mikataba, manunuzi na usimamizi wa miradi ili dhamira ya Mheshimiwa Rais na utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi uende vyema kama tulivyowaahidi Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Katani Ahmed Katani, Mbunge wa Tandahimba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa barabara ya Mtwara – Nanyamba – Tandahimba – Newala – Masasi yenye urefu wa kilometa 210 unatekelezwa kwa awamu ambapo ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Mtwara – Mnivata yenye urefu wa kilomita 50 umekamilika kwa kutumia fedha za ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sehemu ya Mnivata – Newala - Masasi yenye urefu wa kilomita 160, mikataba miwili ya ujenzi chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB)* imesainiwa tarehe 21 Juni, 2023, kwa sehemu za Mnivata – Mitesa yenye urefu wa kilomita 100 na Mitesa – Masasi yenye urefu wa kilomita 60 pamoja na ujenzi wa Daraja la Mwiti. Kwa sasa Makandarasi wa sehemu zote mbili wapo katika hatua za maandalizi ya kuanza ujenzi, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Katani.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa Serikali imefanya uchambuzi yakinifu wa Barabara kutoka Mtama – Mkwiti - Ng'unja – Litehu mpaka Tandahimba miaka mitatu nyuma. Je, lini Serikali itajenga barabara hii kwa kiwango cha lami?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa barabara hii ina kipande korofi cha kutoka Ng'unja kuja Mkwiti. Je, Serikali iko tayari kutenga fedha ya dharura kwa ajili ya kuweka lami kipande kile?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Katani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye upande wa swali la kwanza, ujenzi utaanza lini. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Katani kwa namna ambavyo amefuatilia mpaka Serikali tukafikia hatua ya kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Mara fedha zitakapopatikana ujenzi wa barabara hii utaanza mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kuhusu kipande korofi toka Ng'unja kwenda Mkwiti, Mheshimiwa Mbunge ameomba fedha za dharura. Natumia nafasi hii kuwaelekeza Mameneja wa *TANROADS* Mikoa yote kuangalia maeneo kama haya, maeneo korofi na kuyabainisha na kufanya *assessment* na kuleta Wizarani ili tunapokuwa tunaandaa bajeti, maeneo haya kama aliyoyasema Mheshimiwa Katani tuweze kuyaweka kwenye kipaumbele. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Bilakwate.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE**: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Barabara ya Mrushaka kwenda mpaka Mrongo ilikuwa isainiwe tarehe 24 Agosti, lakini haikusainiwa ni lini barabara hii itasainiwa kwa umuhimu wa wananchi wa Kyerwa na Karagwe? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Innocent Bilakwate, wajina wangu na jirani yangu kule Jimbo la Kyerwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu mara tu Mheshimiwa Rais, aliponiamini na kunileta Wizara hii, moja ya simu niliyoipata ilikuwa ya Mheshimiwa Innocent Bilakwate akiulizia barabara hii.

Nikamwahidi kwamba naomba awe na subira, niape kwanza halafu nitakapokuja ofisini basi tuangalie cha kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kukaa na Mheshimiwa Mbunge na kwa vile hii barabara inapita Jimbo la Karagwe, nimegundua kwa Waheshimiwa Wabunge wengi ipo mikataba ambayo inasubiria kusainiwa kama hii ya Mheshimiwa Bilakwate, kwa hiyo, hatutowachelewesha. Nimeshamwelekeza Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi kufanya haraka iwezekanavyo ili mikataba hii isainiwe, Wakandarasi waanze hatua za ujenzi wa barabara hizi, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa majibu haya tusubiri mikataba isainiwe wote mtapata barabara. *(Kicheko/Makofi)*

Tunaendelea, Mheshimiwa Nashon William.

Na. 101

**Ujenzi kwa Kiwango cha Lami Barabara ya Simbo – Ilagala – Kigoma Kusini**

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi kwa kiwango cha lami Barabara ya Simbo hadi Ilagala?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze, Mbunge wa Kigoma Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu wa barabara ya Simbo – Ilagala – Kalya yenye urefu wa kilometa 234 imeanza kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Daraja la *Lower Malagarasi* ambalo lipo katika barabara hii na kazi zinatarajiwa kukamilika Disemba, 2023. Kuhusu usanifu wa barabara hiyo, Serikali imeanza kutenga fedha kwa ajili ya kuanza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ambapo katika mwaka wa fedha 2023/2024, Mheshimiwa Mbunge tumemtengea shilingi milioni 100 ili kufanya kazi hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nashon.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishukuru Serikali kwa majibu mazuri, lakini nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Daraja la Malagarasi *Lower* litakuwa na kilometa saba za lami.  Je, Serikali haioni haja ya kufanya upembuzi yakinifu haraka wa kipande hiki kidogo cha Simbo - Ilagala chenye kilomita 40? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Nashon, Mbunge wa Kigoma Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya Mheshimiwa Mbunge nimeisikia na Mheshimiwa Mbunge naomba unipe muda ili niweze kufuatilia kipande cha barabara hii ili tuweze kuona lile ambalo linawezekana. Dhamira ya Serikali ni kuhakikisha mitandao yote ya barababara ambayo ipo chini ya *TANROADS,* kwanza zile ambazo hatujafanya upembuzi yakinifu, tunafanya upembuzi yakinifu na kuwa na *database* ili fedha zinapopatikana tu ujenzi wa barabara hizi unaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua pia mahitaji ni mengi ya barabara kujengwa kwa kiwango cha lami, lakini naomba Waheshimiwa Wabunge wanipe muda, nitakaa na timu yangu ya

Wizara lakini kwa kushirikiana na Kamati yetu ya Miundombinu ya Bunge, tuangalie mahitaji haya makubwa na majira haya tunayoingia ambayo Waheshimiwa Wabunge wanafahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeahidi vingi kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan anafanya kila aina ya jitihada fedha zinapatikana, kazi inaenda vizuri, lakini hata mahitaji ambayo bado tutaangalia namna ya kujipanga tukisaidiwa na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati, kaka yangu Kakoso, Makamu Mwenyekiti Mama Anna Kilango, tuangalie *resources* ambazo zinapatikana ndani ya Serikali. Tufanyaje kwa kushirikiana na Waheshimiwa Wabunge ili yale ambayo tuliwaahidi wananchi tuweze kuyatekeleza kwa kiasi kikubwa kadri inavyowezekana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri ametoa majibu ya ujumla. Nakushukuru sana kwa namna unavyoelezea mipango yako.

Tunaendelea, Mheshimiwa Ally Mhata.

Na. 102

**Ahadi Ujenzi wa barabara ya Nangomba hadi Nanyumbu**

**MHE. YAHYA A. MHATA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha ahadi ya ujenzi wa Barabara ya Nangomba hadi Nanyumbu kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ally Yahya Mhata, Mbunge wa Nanyumbu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* tayari imekamilisha kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Barabara ya Nangomba – Nanyumbu yenye urefu wa kilometa 28.32 kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami. Kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mhata.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba niipongeze Serikali kwa jitihada inazofanya katika kuhakikisha miundombinu yetu inakuwa mizuri, lakini naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika barabara hii ninayoitaja ni ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tatu, Mzee wetu Hayati Benjamin William Mkapa, ambaye alikuwa Mbunge wa Jimbo hili ambalo mimi nauliza. Sasa ni miaka 25, Serikali bado inatafuta pesa kwa ajili ya kukamilisha barabara hii. Je, Waziri atakuwa tayari katika mwaka huu kuingiza mpango ili mwaka ujao wa fedha, barabara hii ianze kutengenezwa kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, Mbunge wa Jimbo la Nanyumbu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ningependa nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge kwamba ahadi za viongozi wetu Waheshimiwa Marais Wastaafu na Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, zinatekelezwa, inaweza ikachelewa lakini haimaanishi kwamba hazitatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge ameongea kwa hisia kali hapa kwamba ni miaka 25 toka mpendwa wetu Hayati Rais Mstaafu Benjamin Mkapa ameahidi hatujaanza

utekelezaji wa barabara hii. Nimhakikishie kwamba, nitafuatilia barabara hii ili hata kama tunaanza kidogo, ilimradi tuanze kutekeleza ahadi za Viongozi wetu, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri. Sasa tunakwenda Wizara ya Afya. Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka.

Na. 103

**Idadi ya Madaktari Bingwa nchini**

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA** aliuliza:-

Je, Tanzania ina Madaktari Bingwa Wazalendo wa magonjwa ya binadamu wangapi na katika magonjwa gani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Angelina Adamu Malembeka, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa Tanzania ina jumla ya Madaktari Bingwa Wazalendo 2,469 ambao wamesajiliwa na Baraza la Madaktari Tanganyika kwa fani mbalimbali za Udaktari Bingwa. Kati yao Madaktari Bingwa 2,098 wapo katika Sekta ya Umma na Madaktari Bingwa 371 wapo Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Madaktari hawa wamegawanyika katika maeneo 28 ya Ubingwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Malembeka.

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza maswali mawili ya ziada.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Swali langu la kwanza kwa kuwa Madaktari Bingwa 2,098 wako katika sekta ya umma na Madaktari Bingwa 371 wako katika sekta binafsi; je, Serikali inawapatia marupurupu gani Madaktari Bingwa hao ili kulinda ajira zao wasiende sekta binafsi au nje ya nchi? *(Makofi)*

Swali langu la pili; Je, Serikali ina mpango gani wa kuweza kutambua taaluma bobezi ambazo huwa zinasomewa kwa muda mrefu, waweze kutambua bobezi hizo na kuweka mishahara mikubwa ili kuhamasisha watu waweze kusomea ubobezi huo? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa maswali yake mawili mazuri.

Moja kwanza mpaka sasa kama ambavyo umeona hapa asilimia 75 ya Madaktari wako Serikalini na mpaka sasa Madaktari wengi na watumishi wengi wanapenda zaidi kufanyia kazi Serikalini, maana yake ni kwamba Serikalini kuna uhakika zaidi na *incentive* nyingi zaidi kuliko kwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kama unavyojua kwamba Serikali inatoa *incentive,* mmemsikia Waziri wa Afya akisema kwamba tunatakiwa Madaktari wetu wamekuwa wakikimbia kwenye *private sector* wakati wa jioni wamekuwa wanafanya kazi, kwa hiyo sasa wameruhusiwa ndani ya hospitali zetu za umma wafanye *private clinic* humo humo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niweke vizuri pamoja na hayo yote ambayo Serikali inafanya bado tunafikiri tunahitaji wawe umma

lakini pia wawe *private sector,* kwa hiyo pande zote mbili Madaktari wetu tungefurahi wakafanya kazi sehemu zote, wawe *private sector* wengine wawe *public sector*. Tungefurahi wafanye kote kwa sababu kote wanamhudumia Mtanzania yuleyule.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili ni Je, Serikali inafanya nini kwa wale wanaosoma muda mrefu. Mheshimiwa Waziri wa Afya alipeleka hilo tatizo kwa Mheshimiwa Rais wetu. Mheshimiwa Rais wetu na ameshatoa maelekezo tukae na utumishi ili kujadili kuona Madaktari ambao wanasoma muda mrefu ni kwa namna gani utumishi wakaweka *incentive* au kuongeza mshahara kulingana na ule muda wanaosoma ili wengi wavutiwe kusoma masomo hayo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais wetu ameshatoa maelekeo ya kutatua tatizo hilo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu gani unafanyika kuwapeleka Madaktari Bingwa kama wakiwa wamehamishwa, kwa sababu Mkoa wetu wa Iringa sasa ni karibu mwaka wa tatu Daktari Bingwa wa Mifupa amehamishwa na hatujampata na kuna ajali nyingi sana. Je, ni lini sasa tutampata katika hospitali ya Mkoa wa Iringa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nalichikua tatizo lake kama alivyolisema kuona tunalishughulikiaje, lakini jana Mheshimiwa Waziri wa Afya ameelekeza Idara ya Utumishi wakishirikiana na Idara yetu ta *IT* na kuwasiliana na Utumishi ili tuwe tunaweza kuona kwenye mfumo jinsi ambavyo watumishi wa afya wamegawanyika maeneo mbalimbali na hiyo itaturahisishia kuona ni namna gani, maeneo gani ambayo yana upungufu, ni maeneo

gani wamezidi watumishi kwa namna hiyo tutakuwa tunapanga kwa kujua vizuri wamezidi wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nakubaliana na wewe kwamba Madaktari Bingwa wengi wako Dar es Salaam, wako kwenye Miji mikubwa na Waziri ameshatoa maelekezo kuona namna gani iyo Mikoa ya mbali wanapelekwa hao Madaktari Bingwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani.

Na.104

**Fidia kwa Wahudumu wa Afya wanaopoteza maisha kwa kuhudumia wagonjwa**

**MHE. JACQUILINE N. MSONGOZI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatoa fidia kwa Madaktari na Manesi wanaopoteza maisha wakihudumia Wagonjwa wa Magonjwa ya Mlipuko?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jacqueline Msongozi Ngonyani, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua na kujali mchango mkubwa wa Watumishi wanaohudumia wagonjwa wa magonjwa ya milipuko wakiwemo Madaktari na Wauguzi. Aidha, napenda kufahamisha Bunge lako tukufu kwamba Serikali hutoa fidia kwa watumishi waliofariki kwa sababu za kuwahudumia wagonjwa, wa magonjwa ya mlipuko kwa Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi Sura ya 263, marejeo ya Mwaka 2015 kupitia Mfuko wa

Fidia kwa Wafanyakazi Tanzania. Fidia zinazotolewa ni pamoja na gharama za mazishi na pensheni kwa wategemezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ngonyani.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali naomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini Serikali itafanya mapitio upya ya Sheria Na. 263 ya Mwaka 2015 ili kuongeza fidia na pensheni kwa watumishi hao?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, tatizo hili ni kubwa ambalo linapelekea kwamba Madaktari na Manesi pindi inapotokea magonjwa ya mlipuko wanakosa ari na moyo wa kufanya kazi kutokana na fidia ndogo ambayo wanaipata. Je, Serikali imefanya utafiti wa kina juu ya tatizo kubwa namna hii? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake amabalo kwa kweli linalenga kuboresha huduma lakini kuwatia ari watumishi wa afya. Kwanza, ameuliza kwamba ni lini Serikali itakaa na kujadili ni namna gani tunaweza kuboresha hili. Hili suala linahitaji siyo Wizara ya Afya peke yake linahitaji Wizara mbalimbali za sekta husika kulingana na tatizo lilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niwaombe Wabunge kwa sababu mmelisema hili hapa, basi tutaenda kufanya mawasiliano na kukaa na wenzetu na Serikali ikitokea mjadala ndani ya Serikali ikionekana kuna uhitaji huo basi italetwa hapa Bungeni kwa ajili ya

kubadilisha, lakini turuhusu kwanza likatazamwe na wataalam ili tuone linaweza kufanywajwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili kwamba watumishi wengi wanaogopa kufanya kazi kwenye maeneo yao, kwa sababu wanaogopa kupata matatizo. Mimi nikwambie tu kwanza nitumie fursa hii kuwapongeza watumishi wa afya Tanzania, tulipata tatizo Kagera watumishi wetu hawakutazama kuna hatari gani wakati watu wengine wanakimbia kwenye majanga wao walikimbilia kwenye eneo la tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania Waziri wetu wa Afya alikwenda Marekani juzi kwenye Umoja wa Mataifa walimpongeza kwa kushangaa ni kwa namna gani ndani ya siku 78 Tanzania imeweza ku-*control Marburg*. Maana yake hizi ni juhudi za watumishi wetu hawa ambao wana moyo, wana nia njema ya kuwahudumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnajua wakati wa corona kila mtu alikuwa anakimbia, kila mtu anaogopa kwenda hospitalini lakini watumishi wetu walikimbia na wakafanya na umeona kilichotokea Tanzania na vifo vingi havikuwepo Tanzania kama maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hawa watumishi kwa kweli pamoja na mazingira mengine na matatizo mengine, wanafanya kazi nzuri sana na wana moyo mzuri. Kwa hiyo, nikuambie tu hawaogopi lakini kwa ukweli halisi hebu tukayaangalie haya mengine ambayo umeyasema hapa yaonekane kama kuna sababu ya kufanya hivyo tuende nayo na kuboresha zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais wetu amekuwa akimuelekeza Waziri wetu. Kwa mfano, kuna kijana aliyepata shida kule Kagera na Mheshimiwa Rais wetu alielekeza na yule kijana alipewa zaidi ya Shilingi Milioni Kumi, kama *incentive* tu kupitia masemo wa Mheshimiwa Rais wetu na sasa hivi amaepewa shilingi 10,000,000 yake na anaendelea na shughuli zingine za Kisheria na haki zake za Kisheria bado anaendelea kuzipata. Kwa hiyo,

tutaendelea kuwatia moyo kwa namna hiyo, lakini nikuambie tu kwamba Watumishi wana ari sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Afya.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kwanza kumshuruku Mheshimiwa Naibu Waziri kwa maelezo mazuri, pia nimesimama kumshukuru Mheshimiwa Jacqueline Msongozi kwa swali lake. Nimesimama kwa sababu kipaumbele cha kwanza cha Serikali ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kupambana na magonjwa hatarishi na magonjwa ya mlipuko ni kuwalinda watumishi wa afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatufanyi kitu chochote. Kwanza tunatoa *training* kwa watumishi wa afya jinsi gani ya kuhudumia wagonjwa wa magonjwa ya mlipuko. Pili, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia anatuwezesha kutoa vifaa kinga vya kutosha kwa ajili ya watumishi wa afya, lakini pale kutakapotokea changamoto amesema vizuri Naibu Waziri Serikali inafanya kila linalowezekana kuokoa maisha ya mtumishi wa afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana Kagera tulikuwa na mtumishi Daktari mmoja alipata maambukizi ya *Marburg* kwa sababu ya kumhudumia mgonjwa, tulipeleka *dialysis* mashine Kagera, tumepeleka Madaktari Bingwa Saba na Wauguzi Bingwa na leo Daktari yule tumeweza kuokoa maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimesimama kwanza kuwashukuru watumishi wa afya. Watumishi wetu wa afya siyo waoga, hawajawahi kukimbia wagonjwa. Pili, nimesimama kuwahakikishia Serikali ya Mheshimiwa Rais Samia itatoa kipaumbele cha kuwalinda watumishi wa afya katika kupambana na magonjwa ya mlipuko na magonjwa hatarishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama ili kuweza kuwatia moyo watumishi wa afya, hatujawahi kuona Watumishi wa Afya wamekimbia wagonjwa Tanzania

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana. Tunakupa maua yako wewe, Naibu Waziri pamoja na watumishi wote wa afya. Kwa kweli mtastahili pongezi kubwa sana.

Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Maliasili na Utalii Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah. *(Makofi)*

Na.105

**Kupunguza upoteaji wa uoto wa asili nchini**

**MHE. MOHAMED JUMAH SOUD** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kupunguza upoteaji wa Uoto wa Asili nchini unaosababisha kupoteza hadhi kwa Hifadhi na Mapori ya Akiba?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Jumah Soud, Mbunge wa Donge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu kubwa ya kupotea kwa uoto wa asili katika Hifadhi na Mapori ya akiba ni ongezeko la mimea vamizi katika maeneo hayo. Mimea hiyo husababisha mabadiliko ya aina ya mimea katika maeneo yaliyohifadhiwa kwa kutoa fursa kwa mimea isiyoliwa na wanyamapori kustawi zaidi, kuongezeka na kupunguza uoto wa asili ambao ni tegemeo la wanyamapori. Hadi sasa, tafiti zimebaini aina 47 za mimea vamizi katika maeneo yaliyohifadhiwa. Sababu zinazopelekea kushamiri kwa mimea vamizi ni pamoja na uingizaji wa mifugo kwenye maeneo yaliyohifadhiwa, mabadiliko ya tabianchi, shughuli za binadamu na viumbepori wahamao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jitihada za kudhibiti mimea vamizi, Wizara kupitia Taasisi za uhifadhi inatekeleza mkakati wa

kukabiliana na mimea vamizi katika maeneo hayo ikiwa ni pamoja na kuondoa kwa kung'oa mimea husika katika hifadhi. Aidha, mikakati mingine ni kuimarisha ulinzi wa maeneo yaliyohifadhiwa kwa kudhibiti shughuli za kibinadamu ikiwemo kilimo na uingizwaji wa mifugo hifadhini sambamba na kuwekeza zaidi katika utafiti ili kupata suluhisho la kudumu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Soud Mohammed.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Hifadhi za Taifa, Hifadhi za Misitu pamoja na Mapori ya Akiba, tumeanzisha kwa ajili ya kuhifadhi uoto wa asili na kulinda viumbe hai pamoja na wale ambao wako hatarini kutoweka. Hali kadhalika kwa kuwa hivi karibuni maeneo mengi ya hifadhi na mapori ya akiba, aidha tumeyamega ya kuyateremsha hadhi baadhi yake. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba utaratibu huu wa kumega maeneo na kuteremsha hadhi maeneno ya hifadhi haujirudii tena?

Swali la Pili, kwa kuwa upoteaji wa uoto wa asili unaenda sambamba na upoteaji wa viumbehai, mimea na wanyama ambao wako hatarini kutoweka. Je, Serikali ina mpango gani wa kuainisha na kuwea kutenga utaratibu maalum wa kuweza kuhifadhi viumbe adimu na wale ambao wako hatarini kutoweka? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliridhia kuachia maeneo yenye migogoro vilevile kushusha hadhi baadhi ya mapori na

hifadhi zetu baada ya kubaini kwamba ipo migogoro isiyokuwa na tija iliyokuwa inahatarisha usalama wa wananchi wetu. Serikali ilifanya hivyo baada ya kufanya utafiti wa kina kuona kiasi cha matumizi endelevu ya maeneo hayo, jinsi ambavyo yanaweza kutumika na kama yalikuwa yanatumika kwa jinsi ambavyo ilivyokuwa imekusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale inapoonekana kwamba pori au hifadhi imepoteza sifa yake ya awali ya msingi, basi maeneno hayo hushushwa hadhi na kuwa misitu ili tuweze kuendelea kutunza maeneno haya. Katika kujipanga kuhakikisha kwamba hali hii haijitokezi tena, Serikali inajipanga kutoa elimu kwenye maeneo yote yanayozunguka maeneo ya hifadhi zetu na mapori tengefu ili kujenga uelewa wa wananchi kuhusiana na umuhimu wa rasilimali hizi, vilevile Serikali imejipanga kuongeza doria katika maeneo haya ili uvamizi usijitokeze tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili, Serikali inajitahidi sana kuhakikisha kwamba pale ambapo mimea imetoweka au wanyama wametoweka Serikali imekuja na mkakati wa kupanda miti kwenye maeneo yale yaliyoathirika, kwa mfano kupitia *TFS* tumeaza kupanda miti kule Mkoani Geita, vilevile tumeanza kupanda miti Mkoani Kigoma zaidi ya hekta 139,000 zimepandwa ili kuhakikisha uoto ule haupotei.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pale ambapo tunaona kwamba kuna aina fulani ya wanyama inatoweka, tunakuwa na mkakati wa kuweka maeneo maalum ya kuhakikisha tunadhibiti kuzaliana kwa wanyama wale ili wasije wakatoweka. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jesca.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Hifadhi ya Msitu wa Kihesa - Kilolo pia imekutana na athari hizo. Je, Serikali iko tayari kutusaidia na sisi kuja kupanda miti ili kuendela kuhifadhi eneo lile?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, tumelichukua, wataalam wetu wataenda kufanya tathmini na kuona jinsi ambavyo tunaweza kusaidia.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Mheshimiwa Koka.

Na.106

**Mali za wazee waliopigana Vita Kuu ya Pili ya Dunia chini ya Chama cha *TLC***

**MHE. SILYVESTRY F. KOKA** aliuliza: -

Je, kuna mkakati gani kuhakikisha wazee waliopigana Vita ya Pili ya Dunia chini ya Chama cha *TLC* wananufaika na mali zao?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu: -

Mheshimimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Silyvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwezi Julai, 2022, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iliunda Kamati maalum ya kuchambua na kutoa ushauri kuhusu hatma ya Askari waliopigana Vita Kuu ya Pili ya Dunia mwaka 1939 – 1945 na kuhusu mali za Chama cha Tanzania *Legion & Clubs (TLC)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini hiyo ilibaini kuwa Askari waliopigana Vita Kuu ya Dunia walikuwa 737, kati yao 57 wapo hai na 680 wamekwishafariki. Tathmini ilionesha pia kuwa *TCL* inazo mali zenye thamani ya Shilingi 37,366,323,048.000. Hata hivyo, baadhi ya mali hizo zina madeni na zingine zipo chini ya usimamizi au umiliki wa Taasisi nyingine na hivyo kusababisha mashaka kuhusu umiliki wake.

Katika hali hii, mali zilizothibitishwa kuwa ni za *TLC* bila utata zina thamani ya Shilingi 15,952,574,800. Tathmini ilionesha pia kuwa, maveterani walio hai wanahitaji matunzo ikiwa ni pamoja na bima ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imetoa mapendekezo ya kuuza mali zisizo na utata ambazo nimezitaja za Shilingi 15,952,574,800 na kutoa fidia kwa Maveterani wote walio hai na warithi wa walio fariki. Pia kuwapatia bima ya afya Maveterani walio hai na kuwaenzi Maveterani wote kwa kujenga mnara wa kumbukumbu wa Askari wote waliopigana Vita Kuu ya Pili. Serikali inayafanyia kazi mapendekezo haya na tathmini kuhusu mali zenye utata inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ndiyo mkakati wa Serikali wa kuwaenzi waliopigana Vita ya Pili ya Dunia na kuhakikisha wananufaika na mali zao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Koka.

**MHE. SILYVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu hayo mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mali hizo zenye thamani ya takribani shilingi bilioni 37 ni mali ya Chama cha Wazee Waliopigana Vita ya Pili ya Dunia *(TLC)* ambazo wana haki nazo pamoja na watoto wao kwa mujibu wa katiba yao. Mali hizo zimekodishwa kwa muda mrefu na pesa zinakusanywa, mfano ni Upanga pamoja na kule Tarime, lakini fedha hizo hazijawafikia wale wazee ambao wanaishi kwa shida na wengine wanafariki hata kwa kukosa chakula: Je, ni lini Serikali itahakikisha fedha hizo zinawafikia wazee hao wafaidike nazo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kamati ya Serikali iliyokaa kwenye majadiliano mbalimbali haijawahusisha wazee hao wala watoto wao: Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kupanga siku

maalum ambayo atakutana na Kamati ya Wazee na Watoto hao ili washiriki kufikia maamuzi hayo ambayo Serikali imeyafikia?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie tu kwa ku-*declare* kwamba baba yangu pia ni mmoja wa *veteran* waliopigana Vita ya Pili ya Dunia na sasa hivi ana miaka 103, ana akili timamu na anaulizia sana mali hizo.

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, swali lako lina maslahi ya pesa kwako vilevile, ilibidi useme toka mwanzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kama nilivyojibu kwenye swali langu la msingi, tathmini imeshafanyika na sasa tuko kwenye hatua ya kuhakikisha kwamba tunawafidia wazee hawa. Kwa hiyo, hili linaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu tathmini ya kutowahusisha wazee waliopigana vita na watoto wao, tathmini hii ilikuwa pana na ilihusisha taasisi mbalimbali za Serikali. Bahati mbaya viongozi wa Chama cha *TLC* wote wamefariki, alikuwa amebaki mmoja wakati tathmini inaanza, lakini naye kwa sasa ameshafariki, hata hivyo tulihusisha baadhi ya familia ambazo tuliweza kuzifikia. Kwa hiyo, tathmini iliwahusisha wadau mbalimbali, nafikiri ikiwa nni pamoja na wewe Mheshimiwa Mbunge, tuliweza kupata mawazo yako kwa nyakati mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Khalifa Issa.

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kuna wanajeshi wengi wastaafu waliopigana tokea baada ya uhuru, wamestaafu na mpaka leo wako hai, lakini pensheni zao za mwezi ni ndogo sana: Je, Serikali ina mkakati gani

wa kuwarekebishia ili waweze kukidhi maisha yao? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ni kweli wapo watumishi wa umma ikiwa ni pamoja na wanajeshi wastaafu ambao wamekuwa wakilalamikia pensheni zao kuwa ndogo. Hili ni suala ambalo linafanyiwa kazi kwa pamoja na sekta nyingine zinazohusika na masuala ya pensheni. Kwa hiyo, tutaendelea kuliangalia na kuona ni jinsi gani linaweza kufanyiwa kazi kwa kuzingatia umuhimu wa kazi ambayo wanajeshi hao walifanya na pia kwa kuzingatia uhalisia wa bajeti ya Serikali yetu, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Madini. Mheshimiwa Kisangi, kwa niaba ya Mheshimiwa Ikupa.

Na. 107

**Dar es Salaam kunufaika na madini ujenzi**

**MHE. STELLA I. ALEX K.n.y. MHE. MARIAM N. KISANGI** aliuliza: -

Je, Mkoa wa Dar es Salaam umefaidika vipi na uzalishaji wa madini ya ujenzi yaliyozalishwa katika Mkoa huo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Nasoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba Mkoa wa Dar es Salaam unazalisha na unanufaika na madini ujenzi, hata hivyo wastani wa asilimia 60 ya madini ujenzi yanayotumika kwenye ujenzi wa miradi ya kimkakati katika Mkoa huo yanazalishwa kutokea Mkoa wa Pwani katika Wilaya za Mkuranga, Bagamoyo, Kisarawe na Kibaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, madini ujenzi yanayozalishwa katika Mkoa wa Dar es Salaam yanajumuisha mchanga, kifusi na *limestone*, ambayo yanazalishwa katika Wilaya za Kigamboni, Ilala na Kinondoni. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, makusanyo ya mrabaha na ada ya ukaguzi yatokanayo na madini hayo katika Mkoa wa Dar es Salaam yalifikia kiasi cha shilingi bilioni 1.9.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Madini kupitia Tume ya Madini itaendelea kuimarisha usimamizi katika uzalishaji wa madini ujenzi katika Mkoa wa Dar es Salaam na nchini kote kwa ujumla ili kuongeza manufaa ya madini hayo kwa mwananchi mmoja mmoja na Taifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ikupa.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, Mheshimiwa Kisangi angependa kufahamu ni kwa kiasi gani wananchi kwenye maeneo tajwa wananufaika na uwepo wa madini haya kwa maana ya *CSR*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Stella Ikupa kwa swali lake zuri, kwa sababu manufaa ya wanaokaa katika maeneo yanayochimbwa madini, yako ya aina mbalimbali. Kwa upande wa Serikali kodi zinazokusanywa kutokana na hiyo mirabaha pamoja na ada za ukaguzi zinaingia kwenye Mfuko Mkuu wa Taifa na kuingia kwenye bajeti ambayo kila mwaka Mama Samia anapitisha na miradi

mbalimbali ya maendeleo kama barabara, zahanati na shule zinapata fedha hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa upande wa wawekezaji wenyewe au wenye leseni huwa wanatoa michango kwenye miradi mbalimbali ya jamii katika maeneo hayo, sambamba na kutoa ajira katika maeneo ya migodi. Hivyo, manufaa yapo mengi katika mtizamo huo. Pia wale wanaojiongeza, wanafanya huduma za kuwahudumia wenye migodi kama akina mamalishe wanavyokwenda kupika pale na kutoa huduma mbalimbali.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Nishati. Mheshimiwa Mwambe.

Na. 108

**Umeme wa *REA* Vijiji vya Masasi**

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE** aliuliza:-

Je, lini Vijiji vya Namikunda, Chipole, Machombe, Mtakateni, Machenje, Matawale, Mpekeso, Chakama na Kata ya Temeke vitapewa umeme?

**NAIBU SPIKA:**Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Geoffrey Mwambe, Mbunge wa Masasi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini inatekeleza Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini wa Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili ambapo vijiji vyote ambavyo havina umeme Tanzania Bara vitafikiwa na huduma ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Masasi, Mkandarasi *NAMIS Corporate Limited* alipewa jumla ya vijiji 17 ambavyo havikuwa na umeme. Hadi kufikia tarehe 15 Agosti, 2023, vijiji 11 vimeshawashwa umeme na vijiji sita vitakamilika kabla ya mkataba wa Mkandarasi kwisha tarehe 31 Desemba, 2023. Aidha, vijiji vya Namikunda, Mtakateni, Matawale, Mpekeso na Chakama vimeshawashwa umeme. Vilevile, hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2023, Vijiji vya Chipole na Machombe vitakuwa vimepatiwa umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa zoezi la kusimamisha nguzo katika Kata ya Temeke bado linaendelea na nguzo tayari zimesimamishwa katika Kijiji cha Machenje na zoezi la kuvuta waya linatarajiwa kufanyika mwezi Septemba, 2023. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwambe.

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri. Hata hivyo nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, tuna Kijiji cha Mlundelunde, Kitongoji cha Mchaka ambacho kina shule ya sekondari ambapo bahati mbaya umeme umepita juu yake na shule ile ya sekondari kama taasisi ya Serikali, haijapata ule umeme: Je, nini maelekezo ya Serikali kwa *REA* Mtwara ili waweze kufanya haraka kuunganisha umeme katika hiyo shule ya sekondari?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Tumepata changamoto kubwa kwa Jimbo letu la Masasi Mjini ambapo tuna Kata saba za Sururu, Mwengemtapika, Matawale, Chanikanguo, Temeke, Marika pamoja na Mmbaka ambazo ziko vijijini, lakini wanatakiwa kulipa shilingi 320,000/= kama sehemu ya ada ya uunganishaji wa umeme: Je, Serikali haioni ni wakati muafaka sasa, wananchi hawa wapate haki kwa maana wapo vijijini, waunganishiwe umeme kwa shilingi 27,000/= kama vijiji vingine?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Geoffrey Mwambe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na shule ambayo ameitaja, shule hii ipo katika moja ya kitongoji ambapo utaenda kutekelezwa mradi wa vitongoji 15 ambavyo tayari Serikali imeshatenga fedha kwa mwaka huu wa fedha. Tunaanza kufanya ufuatiliaji ili tuweze kuona ni namna gani tunaanza kutekeleza mradi huu wa vitongoji 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali lake la pili juu ya maeneo ya vijijini ambayo yanakataliwa kutozwa shilingi 27,000/=, tayari Serikali tumeshaya-*identify* haya maeneo na tuko katika mchakato wa mwisho ili kuweza kutolea maelekezo kwa maeneo kama haya ambayo yanaleta mkanganyiko wa bei.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara, jiandae Mheshimiwa Asia.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kule Musoma kuna kijana aliuawa jana kwa sababu alikuwa anapambania mafuta kwenye kituo. Hali ya mafuta kule Tarime ni mbaya, lakini nimesoma kwenye mitandao inasema, Njombe lita moja ni shilingi 7,000. Nimeulizia watu wa Mtwara na maeneo mengine, kule Nyang’ware ni shilingi 6,000, lakini vilevile…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara, wewe ni Mbunge na ulishakuwa Waziri. Waziri anaweza kujibu swali la nyongeza kutokana na swali la msingi. Kaa chini. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Asia.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali la nyongeza. Mkandarasi aliyekabidhiwa vijiji 15 vya Wilaya ya Hanang’ kasi yake

inasuasua sana: Je, nini kauli ya Serikali juu ya Mkandarasi huyu ili kuwapa matumaini wananchi wa Wilaya ya Hanang'?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Asia Halamga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkandarasi aliyekuwepo Hanang' *Nakurwa Investment Company* ni kweli alikuwa anasuasua lakini tumemsimamia na katika vijiji 15 ambavyo vimebakia, vijiji tisa ameshasambaza nguzo, na tuna imani mpaka ifikapo Desemba, 2023 atakuwa amekamilisha kuweka umeme vijiji vyote, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Ameir kwa niaba, Mheshimiwa Londo.

Na. 109

**Wafanyabiashara ambao hawajaingizwa katika mfumo rasmi wa kodi**

**MHE. DENNIS L. LONDO K.n.y. MHE. AMEIR A. AMEIR** aliuliza: -

Je, ni asilimia ngapi ya Wafanyabiashara hawajaingizwa katika Mfumo rasmi wa kodi na Serikali inachukua hatua gani kuwafikia?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ameir Abdalla Ameir, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kupanua wigo wa kodi. Hadi Juni 30, 2023 Mamlaka ya Mapato Tanzania ilikuwa imesajili jumla ya walipa kodi 4,696,999, sawa na asilimia 16 ya idadi ya nguvu kazi iliyopo nchini ambayo ni takribani milioni 33. Idadi ndogo ya usajili wa walipakodi, ikilinganishwa na fursa ya nguvu kazi iliyopo inatokana na sehemu kubwa ya shughuli za kiuchumi hapa nchini kuendeshwa na sekta isiyo rasmi inayokadiriwa kuajiri takribrani watu milioni 27.7.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali kurasimisha sekta isiyo rasmi ni pamoja na kampeni ya mlango kwa mlango inayolenga kuwatambua na kuwasajili wafanyabiashara wasiotambulika, kutenga na kujenga maeneo maalumu ya masoko kwa wafanyabiashara wadogo na kuendelea kutoa elimu na ufafanuzi wa kina kwa wananchi kuhusu masuala ya kodi ili kuhamasisha wananchi kurasimisha biashara na shughuli za kiuchumi kwa hiari, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Londo.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali imekiri kwamba kuna idadi ndogo sana ya usajili kwa maana ni asilimia 16 tu ya nguvu kazi ya walipa kodi: Je, Serikali haioni wakati umefika sasa kwa Wizara ya Fedha, TAMISEMI na Wizara ya Viwanda na Biashara kukaa pamoja na kuona namna bora ya kusajili wafanyabiashara na walipa kodi katika ngazi ya vijiji badala ya kugombania leseni kwa maana ya leseni B?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo ya kimkakati, mfano Jimbo la Mikumi ambalo siyo wilaya wala siyo halmashauri, lakini ni maeneo ya kimkakati ya biashara na kodi: Serikali ina mpango gani wa kuchechemua maeneo haya ili wafanyabiashara washiriki kikamilifu katika ujenzi wa Taifa letu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Ni kweli kama nilivyosema, bado idadi ya walipa kodi ni ndogo na tayari Serikali ina mikakati mbalimbali ili kuhakikisha tunaongeza idadi ya walipa kodi kulingana na nguvu kazi iliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, ni kuendelea kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Ufanyaji Biashara nchini (MKUMBI), na hili tumeendelea kutoa elimu na hatua mbalimbali ambazo zinapelekea kuvutia wafanyabiashara na wazalishaji mbalimbali kurasimisha biashara zao ikiwa ni pamoja na kuondoa kodi, tozo na ada ambazo ni kero kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tumeendelea kuweka mazingira ambayo yanarahisisha usajili wa biashara kwa wananchi wote. Kwa hiyo, tayari Serikali inafanya kazi kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, TAMISEMI lakini pia Wizara ya Viwanda. Sasa hivi tunataka tuone namna ya kuhakikisha tunapeleka maelekezo kwenye ngazi ya vijiji ili kuwa na dirisha la pamoja la kuratibu masuala ya biashara kutoka ngazi ya Kijiji, lakini tayari tumeshafika kwenye halmashauri ambako tunaweka Idara ya Viwanda Biashara na Uwekezaji ambao watafanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, maeneo mkakati, ni kweli tunaona umuhimu wa kuhakikisha maeneo ya kimkakati ambayo yana fursa nyingi za kibiashara kuyawekea miundombinu wezeshi ikiwemo masoko na kuweka vituo maalum vya kuhamasisha wananchi kusajili biashara zao. Tayari Wizara kupitia *BRELA* tumeshaanza kupeleka elimu na kuhamasisha wananchi kusajili biashara zao katika maeneo husika kwa maana ya halmashauri na hata katika maeneo yale ya kimkakati ambayo tunaona yana biashara ambazo zinaweza kuleta tija kwa uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mwendelee kupambana, walipaji kodi asilimia 16 bado ni ndogo sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Mheshimiwa Stela Fiyao.

Na. 110

**Uhitaji wa hati katika maeneo ya umma Songwe**

**MHE. STELLA S. FIYAO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa Hati kwa maeneo yote ya Umma katika Halmashauri za Mkoa wa Songwe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Halmashauri tano za Mkoa wa Songwe, jumla ya maeneo ya umma 1,679 yanatumika kwa ajili ya matumizi mbalimbali kama vile Shule, Zahanati, Vituo vya Afya, Hospitali, Vyuo, Ofisi, Vituo vya Polisi, Mahakama, Maeneo ya Majeshi, Hifadhi za Misitu na Wanyama na Maeneo ya Makumbusho yanayotumiwa na Serikali au Taasisi. Aidha, maeneo 892 yameshapimwa ambapo kati ya hayo, maeneo 637 yameshakamilishwa na kutolewa Hatimilki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuongeza kasi ya umilikishaji wa maeneo ya matumizi ya umma, Serikali imefanya jitihada madhubuti ikiwemo kuondoa au kupunguza baadhi ya gharama za umilikishaji wa maeneo hayo. Hata hivyo, baadhi ya Taasisi za Serikali zikiwemo Halmashauri zetu zimeshindwa kutenga fedha katika bajeti zao kwa ajili ya umilikishwaji wa maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa rai kwa viongozi wa Serikali na Wakuu wa Taasisi nchini wakiwemo viongozi wa Halmashauri za Mkoa wa Songwe kuhakikisha wanatenga fedha katika bajeti zao kwa ajili ya kugharamia upimaji na umilikishwaji wa maeneo yao, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stella.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niwe na maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Swali langu la kwanza, Taasisi nyingi za Umma zimejikita katika kutoa huduma na hazifanyi biashara: Je, Serikali haioni sasa ni muda muafaka kuondoa kodi ya ardhi ili kuziwezesha taasisi nyingi kuweza kupata hati? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, nataka kujua: Ni lini Serikali itakamilisha kutoa hati katika maeneo 787 yaliyosalia katika Halmashauri za Mkoa wa Songwe ili yaweze kupatiwa hati na kuepusha migogoro ya ardhi isiyokuwa na ulazima baina ya wananchi na Serikali? Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Stella, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kuhusu hizi Taasisi za Umma kuziondolea kodi, hili tumelichukua na tutakwenda kulichakata na kuona namna nzuri ya kufanya. Mara nyingi sana taasisi zinazoomba kumilikishwa maeneo haya zinakuwa na makusudio maalum pamoja na miradi maalum. Kwa hiyo, kwao inakuwa ni rahisi sana kutumia vyanzo vyao vidogo kwa ajili ya kumilikishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala la lini maeneo yaliyobaki katika Mkoa wa Songwe yatakwenda kukamilishiwa umilikishwaji wake? Niwaombe hizo taasisi kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, waanze mchakato wa kuomba namna ya umilikishwaji. Hatua zote ziko wazi na taasisi hizo zote zinaelewa utaratibu ambao tumejiwekea katika uratibumzima wa kumilikisha ardhi hapa nchini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sichalwe.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Je, ni lini Wizara ya Ardhi itaingilia kati kutusaidia kutatua migogoro iliyopo ndani Kata ya Kapele kwa kuwafuatilia watu wote ambao wamehodhi na kupora maeneo ya wananchi kinyume na utaratibu bila kuwa hati na wengine kuwa na hati za uwongo kwa kigezo na kusingizia wametumwa na wakubwa huko juu? Ni lini Wizara ya Ardhi mtatusaidia kutatua jambo hili?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Nina nyongeza ndogo kwenye majibu hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa kuzungumza, naomba dakika moja kutoa shukrani. Kwanza, namshukuru sana Mwenyezi Mungu ambae amenipa kibali kuhudumu kwenye Wizara hii ya Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuniteua kuhudumu na kumsaidia kama Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Ninachoweza kumuahidi ni utumishi uliotukuka wa uadilifu. Nitatumikia kwa nguvu zangu na akili zangu zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaliomba Bunge lako tukufu ushirikiano na wakati wote nitakuwa tayari kwa ajili ya kufanya kazi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa nyongeza ndogo ya majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Serikali imejipanga na lipo suala la migogoro ya ardhi. Serikali kupitia Kamati ya Mawaziri Nane ilishafanya utatuzi wa migogoro ya ardhi kwenye vijiji 975.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutumia fursa hii kuwakumbusha Wakuu wa Mikoa 26 yote ya nchi nzima, kuendelea na utekelezaji wa maagizo ya Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwaahidi Waheshimiwa Wabunge ambao wengi tumekutana na wameelezea kero zao akiwemo Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Momba, Mheshimiwa Condester. Baada tu ya Bunge hili kuna mkutano wa Kimataifa Arusha na unaisha Alhamisi, tutajipanga kuanza ziara nchi nzima kutekeleza maagizo ya Baraza la Mawaziri kwenye vijiji 975. Vilevile, kutatua migogoro yote ambayo inajitokeza kwenye maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ushirikiano. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA**: Ahsante kwa majibu sahihi. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Maji. Mheshimiwa Shabani Omary Shekilindi.

Na. 111

**Uhitaji wa maji safi Kata ya Kwekanga – Lushoto**

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** aliuliza: -

Je, lini Serikali itapeleka maji safi na salama katika Kata ya Kwekanga?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi, Mbunge wa Jimbo la Lushoto, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua adha ya maji wanayoipata wakazi wa Kata ya Kwekanga yenye Vijiji vitano vya Kwekanga, Mziragembei, Bombo-Kamghoboro, Mategho na Mshangai. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali katika Mwaka wa fedha 2023/2024, itafanya utafiti wa maji chini ya ardhi *(Hydrogeological survey)* pamoja na kuchimba visima virefu katika Kata za Kwekanga, Kwai, Kilole, Malindi, Makanya na Lushoto Mjini. Kazi hiyo inatarajiwa kufanyika na kukamilika mwezi Disemba, 2023. Uendelezaji wa visima hivyo utafanyika mara baada ya uchimbaji kukamilika na maji kupatikana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shekilindi.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na namshukuru Waziri kwa majibu mazuri. Changamoto ya kukosa maji katika Kata ya Kwekanga, Kwai, Malibwi, Mbwei, Makanya na Mlola ni changamoto muda mrefu sana. Suala hili nimeliongelea zaidi ya takribani Mikutano Kumi bila mafanikio yoyote na wananchi wangu wakiendelea kupata tabu ya maji.

Je, nini mkakati wa dharura wa Serikali kupeleka gari la kuchimba visima katika kata nilizozitaja?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kuna Mradi wa Magamba eneo la Gelwa Ali unaitwa Mtaa Na. 9 na *survey* imeshafanyika. Mradi ule ukikamilika unakwenda kuhudumia kata zaidi 13. Je, ni lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kutekeleza mradi huo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Shekilindi, amekuwa mfuatiliaji nilikuahidi nitafika jimboni Mheshimiwa Mbunge, kipindi kilichopita sikuweza, baada ya Bunge hili nitahakikisha tunakwenda kuona maeneo haya na kuweka msisitizo ili kuhakikisha miradi hii inatekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa dharura tayari Mheshimiwa Mbunge tumekutengea shilingi milioni 300. Tunataka baada ya ukamilishaji wa hii *survey* visima hivi vichimbwe na hatutaishia tu kuchimba visima. Tutahakikisha tunasambaza na kujenga vichotea maji kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, fedha za Miradi ya Mbao tayari usanifu umekamilika. Mheshimiwa Mbunge, tayari tutaendelea kukuletea fedha. Sasa hivi tumekutengea milioni 300 na mgao ujao tutahakikisha tunakutengea fedha. Mimi mwenyewe nitakuja jimboni kuleta msukumo hii miradi iweze kutekelezeka.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Hoja ya kuahirisha Shughuli za Bunge.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, kaa chini. *(Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Nimekaa *boss.*

**NAIBU SPIKA:** Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, wageni waliokaa jukwaa la Spika.

Wageni 10 wa Spika, Mheshimiwa, Dkt. Tulia Ackson kutoka *Tanganyika Law Society (TLS),* wakiongozwa na Rais wao, Ndugu Harold Sungusia. *(Makofi)*

Wengine ni Ndugu Christopher Mageka, Ndugu Edward Heche, Ndugu Irene Mwakyusa, Ndugu Thomas Matatizo Msasa,

Ndugu Steven Kitale, Ndugu John Nyange, Ndugu Mariam Othman, Ndugu Nelson Frank na Ndugu Prisca Chogero. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wageni sita wa Naibu Waziri, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamis ambao ni Wanasayansi na Wataalam wa Maabara kutoka Mjini Magharibi Zanzibar. *(Makofi)*

Wageni 22 wa Mheshimiwa Jumanne Kishimba ambao ni Madiwani kutoka Kahama Mjini, Mkoa wa Shinyanga. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Khamis Kasim Ali ambaye ni mpiga kura wake kutoka Mgogoni, Mkoa wa Kusini Pemba, Ndugu Abdulrahim Kombo. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Christina Mzava, mdogo wake kutoka Mkoa wa Shinyanga, Ndugu Frida Betty. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Omar Ali Omar ambao ni familia yake kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Fatma Toufiq ambao ni walimu wa Shule ya Sekondari Buigiri na Shule ya Msingi Uguzi kutoka Chamwino, Mkoa wa Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Janeth Mawahanga ambao ni ndugu zake kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ambaye ni jamaa yake kutoka Mpwapwa, Mkoa wa Dodoma. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Robert Maboto ambao ni familia yake kutoka Bunda, Mkoa wa Mara wakiongozwa na mama yake mzazi, Ndugu Maria Maboto. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Regina Qwaray ambao ni wapiga kura wake kutoka Mererani, Simanjiro Mkoa wa Manyara. *(Makofi)*

Wageni sita wa Mheshimiwa Boniphace Butondo ambao ni Madiwani kutoka Kishapu, Mkoa wa Shinyanga. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wanafunzi 120 na walimu 31 kutoka Shule ya Awali na Msingi Ndetembia Matemu kutoka Mkoa wa Morogoro. *(Makofi)*

Wanafunzi 62 na walimu 15 wa Shule ya Msingi *DCT Holy Trinity ya* Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Mgeni kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Ndugu Abednego Luhalala, karibu sana Dodoma. *(Makofi)*

Katibu.

**MBUNGE FULANI:** Hoja ya kuahirisha shughuli za Bunge

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI.**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3 ya Mwaka 2023 *(The Written Laws Miscellaneous Amendment (No. 3) Bill of 2023)***

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2023 *(The Written Laws Miscellaneous Amendment (No. 3) Bill of 2023)* umekwishasomwa kwa mara ya kwanza Bungeni. Mara baada ya hatua hiyo na kwa mamlaka niliyonayo chini ya Kanuni 97(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Sasa,

naelekeza Muswada huo ufanyiwe kazi na Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria kwa muda huu.

Waheshimiwa Wabunge, niwaombe. Tunasitisha Bunge kwa muda wa saa moja. Sasa hivi ni saa 04,30 itakapofika saa 05.20 Waheshimiwa Wabunge wote turudi kwenye viti vyetu leo. Nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa tano na nusu.

*(Saa 4.30 Asubuhi Bunge Lilisitishwa hadi Saa 05.30 Asubuhi)*

*(Saa 5.30 Asubuhi Bunge Lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na: -

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:**

Maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2023 *(The Written Laws Miscellaneous Amendment (No. 03) Act of 2023)*.

**MHE MASHIMBA M. NDAKI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:**

Taarifa ya Kamati hii kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) ya Mwaka 2023 *(The Written Laws Miscellaneous Amendment (No. 3) Bill of 2023)*.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) ya Mwaka 2023 *(The Written Laws Miscellaneous Amendment (No.3) Bill of 2023)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, sasa namwita mtoa hoja.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu, kuwasilisha Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali (Na. 3) ya Mwaka 2023 *(The Written Laws Miscellaneous Amendment (No. 3) Bill of 2023)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuiongoza nchi kwa malengo, ujasiri na uzalendo wa hali ya juu.

Naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge pamoja na wananchi wenzangu kuendelea kumuomba Mwenyezi Mungu amjale Rais wetu kila la heri katika kuliongoza Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa Mbunge, na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mawaziri wote kwa kazi kubwa wanayoifanya

katika kuwaletea maendeleo wananchi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuungana na Watanzania wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri Mkuu. Pia namtakia kila la heri katika kutekeleza majukumu yake katika nafasi hiyo. Ni wazi kuwa dhamana aliyopewa na imani ambayo Mheshimiwa Rais ameiweka kwake inaakisi uaminifu na umahiri wake katika utendaji wa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru Mawaziri wote kwa ushirikiano wanaoipatia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kutekeleza majukumu yake. Aidha, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wewe mwenyewe Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuendelea kuongoza na kusimamia vikao na mijadala ndani ya Bunge letu kwa umahiri na kwa kuzingatia Sheria na Kanuni zinazoliongoza Bunge hili. Ninawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao wa kikatiba wa kutunga sheria pamoja na kuisimamia Serikali. Ninaishukuru Ofisi ya Bunge ikiongozwa na Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa Joyce Mwihambi, *ndc,* na watumishi wote wa Bunge kwa ushirikiano mnaoipatia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote walioteuliwa katika Wizara mbalimbali. Ninawatakia kila la kheri katika kutekeleza majukumu yenu mapya. Ofisi yangu inaahidi kuwapa ushirikiano wa kutosha katika kulitumikia Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee napenda kumpongeza Mheshimiwa Pindi Hazara Chana kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri wa Katiba na Sheria. Kwa niaba ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ninapenda kumhakikishia ushirikiano wa hali ya juu katika kutekeleza majukumu yake mapya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakiongozwa na aliyekuwa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dkt. Evaristo Emmanuel Longopa, kwa kuendelea kutekeleza vyema majukumu na kazi za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Nichukue fursa hii pia kumpongeza Dkt. Evaristo Emmanuel Longopa kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais na kuteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania. Ninamtakia utekelezaji mwema wa majukumu yake. Aidha, naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali mteule Prof. Kennedy Gastorn kwa kuaminiwa na kuteuliwa kushika nafasi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie shukrani zangu kwa kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Madaba na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mbunge wa Nkenge kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia wakati wa kupitia Muswada huu katika Kamati. Kamati hii ilifanya kazi kubwa na nzuri ya kuchambua Muswada huu kwa makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Namba Tatu wa Mwaka 2023 kama ulivyowasilishwa unapendekeza marekebisho katika Sheria zifuatazo:

(1) Sheria ya Kanda Maalum za Uwekezaji kwa ajili ya Mauzo Nje ya Nchi, Sura ya 373 (*The Export Processing Zones Act, Cap. 373*); na

(2) Sheria ya Kanda Maalum za Kiuchumi, Sura ya 420 (*The Special Economic Zones Act, Cap. 420)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Tatu. Sehemu ya Kwanza inahusu masharti ya utangulizi ambayo yanajumuisha jina la sheria inayopendekezwa kutungwa na namna ambavyo sheria mbalimbali zimerekebishwa katika muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Pili na Sehemu ya Tatu za Muswada zinapendekeza kurekebisha Sheria ya Kanda Maalum za Uwekezaji kwa ajili ya Mauzo Nje ya Nchi, Sura ya 373 na Sheria ya Kanda Maalum za Kiuchumi, Sura ya 420. Sheria hizi zinarekebishwa katika vifungu vya pili na tatu, mtawalia kwa kufuta na kuandika upya tafsiri ya neno "Waziri". Aidha, sambamba na marekebisho ya tafsiri ya neno Waziri, kifungu cha 14 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kufuta maneno *"responsible for industries"*. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuhakikisha kuwa Sheria husika zinatekelezwa na Waziri mwenye dhamana na masuala husika kwa mujibu wa Hati idhini ya Mgawanyo wa Majukumu ya Mawaziri ambayo hutolewa na Rais. Kwa sasa, sheria hizi zinamtafsiri Waziri kama Waziri mwenye dhamana ya viwanda, ilhali jukumu la usimamizi wa masuala haya limehamishiwa Ofisi ya Rais - Mipango na Uwekezaji. Hatua hii itaondoa ulazima wa kufanya marekebisho katika sheria kila yanapotokea mabadiliko katika Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2023, ninaomba kutoa hoja kwamba Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Namba tatu wa Mwaka 2023 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Bill, 2023]* ujadiliwe na kupitishwa katika hatua ya Kusomwa kwa Mara ya Pili na ya Tatu na hatimaye marekebisho yanayopendekezwa yawe sehemu ya Sheria za Nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**HOTUBA YA MHESHIMIWA JAJI DKT. ELIEZER MBUKI FELESHI, MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI AKIWASILISHA MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI (Na. 3) WA MWAKA 2023 (THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (No. 3) BILL, 2023) KATIKA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako tukufu kuwasilisha Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2023 (The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Bill, 2023).

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie nafasi hii kumpongeza Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuiongoza Nchi kwa malengo, ujasiri na uzalendo wa hali ya juu. Naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge na Wananchi wenzangu kuendelea kumwomba Mwenyezi Mungu amjaalie Rais wetu kila la kheri katika kuliongoza Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza Mhe. Dkt. Philip Isdory Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mawaziri wote kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuwaletea maendeleo wananchi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, napenda kuungana na Watanzania wenzangu kumpongeza Mhe. Dkt. Doto Mashaka Biteko kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri Mkuu. Pia ninamtakia kila la kheri katika kutekeleza majukumu yake katika nafasi hiyo. Ni wazi kuwa dhamana aliyopewa na imani ambayo Mhe. Rais ameweka kwake inaakisi uaminifu na umahiri wake katika utendaji kazi.

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru Mawaziri wote kwa ushirikiano wanaoipatia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kutekeleza majukumu yake. Aidha, napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza wewe mwenyewe, Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuongoza na kusimamia vikao na mijadala ndani ya Bunge letu kwa umahiri na kwa kuzingatia Sheria na Kanuni zinazoliongoza Bunge hili. Ninawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao wa Kikatiba wa kutunga sheria pamoja na kuisimamia Serikali.

Ninaishukuru Ofisi ya Bunge ikiongozwa na Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa Joyce Mwihambi, (ndc.) na watumishi wote wa Bunge kwa ushirikiano mnaoipatia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote walioteuliwa katika Wizara mbalimbali. Ninawatakia heri katika kutekeleza majukumu yenu mapya. Ofisi yangu inaahidi kuwapa ushirikiano wa kutosha katika kulitumikia Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee napenda kumpongeza Mhe. Pindi Hazara Chana kwa kuteuliwa na Mhe. Rais kuwa Waziri wa Katiba na Sheria. Kwa niaba ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ninapenda kumhakikishia ushirikiano wa hali ya juu katika kutekeleza majukumu yake mapya.

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakiongozwa na aliyekuwa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dkt. Evaristo Emanuel Longopa, kwa kuendelea kutekeleza vyema majukumu na kazi za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Nichukue fursa hii pia kumpongeza Dkt. Evaristo Emanuel Longopa kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais na kuteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania. Ninamtakia utekelezaji mwema wa majukumu yake. Aidha, naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali mteule

Prof. Kennedy Gastorn kwa kuaminiwa na kuteuliwa kushika nafasi hiyo.

Mheshimiwa Spika, nimalizie shukrani zangu kwa kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria inayoongozwa na Mhe. Dkt. Joseph Kizito Mhagama (Mbunge wa Madaba) na Makamu Mwenyekiti Mhe. Florent Laurent Kyombo (Mbunge wa Nkenge) kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia wakati wa kupitia Muswada huu katika Kamati. Kamati hii ilifanya kazi kubwa na nzuri ya kuchambua Muswada huu kwa makini.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2023 kama ulivyowasilishwa unapendekeza marekebisho katika Sheria zifuatazo:

1. Sheria ya Kanda Maalum za Uwekezaji kwa ajili ya Mauzo Nje ya Nchi, Sura ya 373 (The Export Processing Zones Act, Cap. 373); na

2. Sheria ya Kanda Maalum za Kiuchumi, Sura ya 420 (The Special Economic Zones Act, Cap. 420).

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Tatu. Sehemu ya Kwanza inahusu Masharti ya Utangulizi ambayo yanajumuisha jina la sheria inayopendekezwa kutungwa na namna ambavyo sheria mbalimbali zimerekebishwa katika Muswada.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili na Sehemu ya Tatu za Muswada zinapendekeza kurekebisha Sheria ya Kanda Maalum za Uwekezaji kwa ajili ya Mauzo Nje ya Nchi, Sura ya 373 na Sheria ya Kanda Maalum za Kiuchumi, Sura ya 420. Sheria hizi zinarekebishwa katika vifungu vya 2 na 3, mtawalia kwa kufuta na kuandika upya tafsiri ya neno "Waziri". Aidha, sambamba na marekebisho ya tafsiri ya neno Waziri, kifungu cha 14 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kufuta maneno "responsible for industries". Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuhakikisha kuwa Sheria husika zinatekelezwa na Waziri mwenye dhamana na masuala husika kwa

mujibu wa Hati Idhini ya Mgawanyo wa Majukumu ya Mawaziri ambayo hutolewa na Rais. Kwa sasa, Sheria hizi zinamtafsiri Waziri kama Waziri mwenye dhamana ya viwanda, ilhali jukumu la usimamizi wa masuala haya limehamishiwa Ofisi ya Rais - Mipango na Uwekezaji. Hatua hij itaondoa ulazima wa kufanya marekebisho katika Sheria kila yanapotokea mabadiliko katika Wizara.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2023, ninaomba kutoa hoja kwamba Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2023 (the Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Bill, 2023) ujadiliwe na kupitishwa katika hatua ya Kusomwa kwa Mara ya Pili na ya Tatu na hatimaye marekebisho yanayopendekezwa yawe sehemu ya Sheria za Nchi.

Mheshimiwa Spika, NAOMBA KUTOA HOJA

Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi (Mb)
MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja imetolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono, sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Namba Tatu wa Mwaka 2023 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.3) Bill, 2023]*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utangulizi, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3 wa Mwaka 2023 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.3] Bill, 2023)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 93(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Muswada huu umesomwa Bungeni kwa mara ya kwanza katika Mkutano wa Kumi na Mbili, Kikao cha Saba kwenye Bunge la 12, leo tarehe 6 Septemba, 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 97(1) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 136(14) na Kifungu cha 7(1)(b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, uliuelekeza Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ili ufanyiwe uchambuzi na kujadiliwa mapema iwezekanavyo. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, Kamati imeuchambua na kuujadili Muswada huu kwa kuzingatia, Katiba, sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza jukumu hilo Kamati ilikutana na Serikali mapema leo na kupokea maelezo ya Mheshimiwa Jaji Eliezer Mbuki Feleshi (Mb), Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu maudhui ya Muswada huu. Baada ya Kamati kupatiwa maelezo ya Serikali, Wajumbe walipata fursa ya kuuliza maswali, na kupata maelezo ya ufafanuzi katika ibara mbalimbali za Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hatua hiyo, Kamati ilijadili maudhui ya Muswada kwa kuzingatia maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na ilizingatia masharti ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge na kukujulisha rasmi kwamba Kamati imekamilisha uchambuzi wa Muswada ili ujadiliwe Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchambuzi wa Muswada, Kamati iliuchambua Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria

Mbalimbali Namba tatu wa Mwaka 2023 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.3) Bill, 2023]* ukiwa umegawanyika katika sehemu kuu tatu na unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria mbili kwa madhumuni ya kuondoa upungufu au kutatua changamoto ambazo zimejitokeza katika utekelezaji wa sheria hizo. Sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni zifuatazo: -

(a) Sheria ya Kanda Maalum za Uwekezaji kwa ajili ya Mauzo Nje ya Nchi, Sura 373 *(The Export Processing Zones Act, (Cap. 373));* na

*(b)* Sheria ya Kanda Maalum za Kiuchumi, Sura ya 420 *(The Special Economic Zones Act, (Cap. 420))*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Kwanza ya Muswada ambayo inahusu masharti ya utangulizi, inajumuisha Ibara ya kwanza yenye jina fupi na Ibara ya pili inayoeleza marekebisho yanayofanyika katika sheria mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la sheria zinazofanyiwa marekebisho na maudhui yake, wakati wa kufanya uchambuzi wa Muswada huu, pamoja na maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Seriakali Kamati ilifahamishwa kuwa, Sehemu ya Pili na ya Muswada inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Kanda Maalum za Uwekezaji kwa ajili ya Mauzo Nje ya Nchi, Sura 373 *[The Export Processing Zones Act, (Cap. 373)]*. Marekebisho hayo yanafafanuliwa katika Ibara ya tatu hadi Ibara ya tano ya Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya nne ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika sehemu ya tafsiri kwa kufuta tafsiri ya neno "*Minister*" yenye maana ya Waziri mwenye dhamana na masuala ya viwanda, na badala yake kuandika tafsiri mpya ya neno "*Minister*" yenye maana ya Waziri mwenye dhamana na masuala ya kanda za uwekezaji kwa ajili ya mauzo nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya tano ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 14(2)(a) kwa kufuta maneno "*responsible for industries*". Lengo la marekebisho hayo ni kumuondoa Waziri mwenye dhamana na masuala ya viwanda kama mjumbe wa Bodi ya Mamlaka ya Kanda Maalum za Uwekezaji kwa ajili ya mauzo nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya tatu ya Muswada inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Kanda Maalum za Kiuchumi, Sura ya 420 *[The Special Economic Zones Act, (Cap. 420)]*. Marekebisho hayo yanafafanuliwa katika Ibara ya 6 na 7 ya Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ibara ya saba ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika sehemu ya tafsiri kwa kufuta tafsiri ya neno "*Minister*" yenye maana ya Waziri mwenye dhamana na masuala ya viwanda, na badala yake kuandika tafsiri mpya ya neno "*Minister*" yenye maana ya Waziri mwenye dhamana na masuala ya kanda maalum za kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imeridhika kwamba, marekebisho yanayopendekezwa yatasaidia utekelezaji bora wa sheria zinazohusika na kwamba yamezingatia hati idhini ya mgawanyo wa majukumu ya Mawaziri ambayo hutolewa na Rais. Kwa sasa sheria hizi zinamtafsiri Waziri kama Waziri mwenye dhamana ya Viwanda, ilhali jukumu la usimamizi wa masuala haya limehamishiwa Ofisi ya Rais – Mipango na Uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati; Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Muswada yanayowasilishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuwa yanalenga kuhakikisha kuwa sheria zinazorekebishwa zinaendana na muundo na majukumu kulingana na Hati Idhini ya mgawanyo wa majukumu ya Mawaziri iliyotolewa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 22 Juni, 2023 katika Gazeti la Serikali Namba 407(b); ambayo inaeleza kuwa majukumu ya usimamizi wa masuala ya uwekezaji ambayo awali

yalikuwa kwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji sasa yanahamishiwa Ofisi ya Rais – Mipango na Uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii ya kuleta marekebisho haya muhimu kwa lengo la kuboresha ufanisi na uendeshaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais – Mipango na Uwekezaji. Kamati inaona kuwa ni muhimu kuhakikisha kuwa sheria zetu zinakwenda sambamba na mabadiliko ya kiutendaji Serikalini ili kuleta tija na ustawi kwa Wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, shukrani, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati kwa kuujadili na kuuchambua Muswada huu ili kuboresha maudhui yaliyomo katika marekebisho yanayopendekezwa. Kwa umuhimu wa mchango wao katika kushughulikia Muswada huu, naomba niwatambue kwa orodha nzima kuingia kwenye Hansard ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Eliezer Mbuki Feleshi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, pamoja na watendaji wote wa Serikali kwa ushirikiano wao wa dhati kwa kuyapokea maoni ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* na kwa upekee Sekretarieti ya Kamati kwa uratibu wa shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja, baada ya kusema hayo, Kamati inalishauri Bunge lako Tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha Muswada huu kama lilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

**6 SEPTEMBA, 2023**

# MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI NA. 3 WA MWAKA 2023 *[THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO.3) BILL, 2023]* – KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI

---

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Awali na Hadidu za Rejea

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3 wa Mwaka 2023 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.3) Bill, 2023)*.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 93 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Muswada huu umesomwa Bungeni kwa mara ya kwanza katika Mkutano wa kumi na mbili, kikao cha saba kwenye Bunge la 12, leo tarehe 06 Septemba, 2023.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 97 (1) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 136 (14) na Kifungu cha 7(1) (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, uliuelekeza Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ili ufanyiwe uchambuzi na kujadiliwa mapema iwezekanavyo. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kwamba, Kamati imeuchambua na kuujadili Muswada huu kwa kuzingatia, Katiba, Sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

### 1.2 Namna Kamati ilivyotekeleza Jukumu la Uchambuzi wa Muswada

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilikutana na Serikali mapema leo na kupokea maelezo ya Mhe. Jaji Eliezer Mbuki Feleshi (Mb) Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu maudhui

ya Muswada huu. Baada ya Kamati kupatiwa maelezo ya Serikali, Wajumbe walipata fursa ya kuuliza maswali, na kupata maelezo ya ufafanuzi katika ibara mbalimbali za Muswada.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya hatua hiyo, Kamati ilijadili maudhui ya Muswada kwa kuzingatia maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na nilizingatia masharti ya Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge na kukujulisha rasmi kwamba Kamati imekamilisha uchambuzi wa Muswada ili ujadiliwe Bungeni.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MUSWADA

### 2.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilichambua Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.3 wa Mwaka 2023 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.3) Bill, 2023]* ukiwa umegawanyika katika sehemu kuu Tatu (3) na unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria mbili (2) kwa madhumuni ya kuondoa upungufu au kutatua changamoto ambazo zimejitokeza katika utekelezaji wa Sheria hizo. Sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni zifuatazo: -

(a) Sheria ya Kanda Maalum za Uwekezaji kwa ajili ya Mauzo Nje ya Nchi, Sura 373 (The Export Processing Zones Act, (Cap. 373)); na

(b) Sheria ya Kanda Maalum za Kiuchumi, Sura ya 420 (The Special Economic Zones Act, (Cap. 420)).

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Kwanza ya Muswada ambayo inahusu masharti ya utangulizi, inajumuisha **Ibara ya 1** yenye jina fupi na **Ibara ya 2** inayoeleza marekebisho yanayofanyika katika sheria mbalimbali.

## 2.2 Sheria Zinazofanyiwa Marekebisho na Maudhui yake

**Mheshimiwa Spika**, Wakati tunafanya uchambuzi wa Muswada huu Pamoja na Maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Seriakali, Kamati ilifahamishwa kuwa, Sehemu ya Pili na ya Muswada inapendekeza marekebisho ya **Sheria ya Kanda Maalum za Uwekezaji kwa ajili ya Mauzo Nje ya Nchi, Sura 373 (The Export Processing Zones Act, (Cap. 373)).** Marekebisho hayo yanafafanuliwa katika Ibara ya 3 hadi Ibara ya 5 ya Muswada.

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 4** ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika sehemu ya tafsiri kwa kufuta tafsiri ya neno "*Minister*" yenye maana ya Waziri mwenye dhamana na masuala ya Viwanda, na badala yake kuandika tafsiri mpya ya neno "*Minister*" yenye maana ya Waziri mwenye dhamana na masuala ya Kanda za Uwekezaji kwa ajili ya Mauzo Nje ya Nchi.

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 5** ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 14(2)(a) kwa kufuta maneno "*responsible for industries*". Lengo la marekebisho haya ni kumuondoa Waziri mwenye dhamana na masuala ya Viwanda kama mjumbe wa Bodi ya Mamlaka ya Kanda Maalum za Uwekezaji kwa ajili ya Mauzo Nje ya Nchi.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza marekebisho ya **Sheria ya Kanda Maalum za Kiuchumi, Sura ya 420 (The Special Economic Zones Act, (Cap. 420)).** Marekebisho hayo yanafafanuliwa katika Ibara ya 6 na 7 ya Muswada.

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 7** ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika sehemu ya tafsiri kwa kufuta tafsiri ya neno "*Minister*" yenye maana ya Waziri mwenye dhamana na masuala ya Viwanda, na badala yake kuandika tafsiri mpya ya neno "*Minister*" yenye maana ya Waziri mwenye dhamana na masuala ya Kanda Maalum za Kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeridhika kwamba, marekebisho yanayopendekezwa yatasaidia utekelezaji bora wa Sheria zinazohusika na kwamba yamezingatia hati idhini ya mgawanyo wa majukumu ya Mawaziri ambayo hutolewa na Rais. Kwa sasa Sheria hizi zinamtafsiri Waziri kama Waziri mwenye dhamana ya Viwanda, ilihali jukumu la usimamizi wa masuala haya limehamishiwa Ofisi ya Rais – Mipango na Uwekezaji.

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Muswada yaliyowasilishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuwa yanalenga kuhakikisha kuwa Sheria zinazorekebishwa zinaendana na muundo na majukumu kulingana na Hati Idhini ya mgawanyo wa majukumu ya Mawaziri iliyotolewa na **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** tarehe 22 Juni, 2023 katika **Gazeti la Serikali Na. 407B** ambayo inaeleza kuwa majukumu ya usimamizi wa masuala ya uwekezaji ambayo awali yalikuwa kwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji sasa yanahamishiwa Ofisi ya Rais - Mipango na Uwekezaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii ya kuleta marekebisho haya muhimu kwa lengo la kuboresha ufanisi na uendeshaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais - Mipango na Uwekezaji, Kamati inaona kuwa ni muhimu kuhakikisha kuwa sheria zetu zinakwenda sambamba na mabadiliko ya Kiutendaji Serikalini ili kuleta tija na ustawi kwa Wananchi.

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati kwa kuujadili na kuuchambua Muswada huu ili kuboresha maudhui yaliyomo katika marekebisho yanayopendekezwa. Kwa umuhimu wa mchango wao

katika kushughulikia muswada huu, naomba niwatambue kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Florent Laurent Kyombo, Mb – **M/Mwenyekiti**
2. Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb - Mjumbe
3. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Boniphace Nyangindu Butondo, Mb- Mjumbe
6. Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Omar Issa Kombo, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Salum Mohammed Shaafi, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Agnesta Lambert Kaiza, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Khadija Shaaban Taya, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Jonas Van Zeeland, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Abeid Ighondo Ramadhani, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Tumaini Bryceson Magessa, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, Napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mhe. Eliezer Mbuki Feleshi Mwanasheria Mkuu wa Serikali, pamoja na watendaji wote wa Serikali kwa ushirikiano wao wa dhati kwa kuyapokea maoni ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* na kwa upekee Sekretarieti ya Kamati kwa uratibu wa shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

### 4.2 Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, Kamati inalishauri Bunge lako tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha Muswada huu kama lilivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Mhe. Joseph Kizito Mhagama (Mb)
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA**

6 Septemba, 2023

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa sasa tunaanza mjadala tunaanza na Mheshimiwa Khadija Taya, Mheshimiwa Shangazi jiandae Mheshimiwa Ole Ieika, Mheshimiwa Khadija.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii kuchangia Muswada huu. Kwanza naomba niungane na wenzangu kuwapongeza Mawaziri wote walioteuliwa, sana sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu. Lakini vilevile nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuzidi kuwaamiani vijana katika majukumu makubwa kabisa ya nchi hii. Hii inaongeza chachu lakini inatupa moyo sana vijana, pia inatuamsha kuona kwamba tunaweza kushika nafasi kubwa *especially* ukimtaja Mheshimiwa Juduth Kapinga, kwa kweli hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama unavyofahamu tuko hapa kwa ajili ya kubadilisha sheria tukiamini kwamba hizi sheria zinaenda kufanya kazi. Kwa hiyo kama sheria haitoweza kwenda kufanya kazi maana yake lengo kuu lazima tubadilishe au turekebishe ili tuweze kusaidia wananchi au tusaidie jamii yetu. Mheshimiwa Rais ameona fika kabisa, na juzi amebadilisha Mawaziri na ameweza kubadilisha Wizara na kutengeneza Wizara mpya ambayo ni Wizara ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. Hii Wizara imepewa majukumu makubwa sana ya kufanya. Lakini kama unavyoweza kuona kwamba kuna baadhi ya majukumu yalikuwa yamebakia katika Wizara ya Viwanda na Biashara sasa leo hii wameona kuna umuhimu wa kubadilisha kuona *EPZ* ihamie kwenye Wizara ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu sote kwamba *EPZ* ni sheria ya uwekezaji ya masuala ya mauzo ya nje ya nchi. Kwa hiyo Mheshimiwa Rais anauwezo wa kuipeleka hii sehemu yoyote, na ndio maana lengo la Sheria hii kubadilishwa ni ili iweze kwenda katika Wizara nyingine yoyote. Kama leo hii *EPZ* ikiamua kwenda Wizara ya Viwanda na Biashara basi iweze kufanya kazi, ndilo lengo kuu la mabadiliko ya sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba sana nimpongeze Mheshimiwa Rais, na pia niipongeze Serikali kwa kutuletea sheria hii ambayo inatupa *flexibility,* kwamba hatutakuwa tunabadili mara kwa mara; leo hii *EPZ* imeenda Wizara nyingine basi tubadilishe sheria kupeleka Wizara nyingine, lakini inatupa uwanja mpana wa kusema sasa *EPZ* ipo wizara fulani basi sheria hii iweze kwenda vizuri na iweze kwenda kufanya kazi katika Wizara yoyote ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kwa mabadiliko hayo tunaomba tuipongeze Serikali lakini tupongeze pia Kamati, kwa sababu Kamati katika mchango wake iliona pia kuna pengo la Katibu Mkuu kutokuwepo katika Kamati hii ya *EPZ* Katibu Mkuu wa Wizara rasmi, hivyo basi Serikali imetuahidi kwamba itaweza kuleta marekebisho mengine ambayo haya marekebisho yataweza kuja kusaidia ili Katibu Mkuu wa Wizara hii ambaye ndio *permanent secretary* wa Waziri aweze kujua vizuri masuala yote ya *EPZ* kuliko kwenda kumchukua Mheshimiwa Waziri awe kila siku anampelekea taarifa ya kikao cha Kamati ambayo mambo ambayo yameelezewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa kusema hayo nashukuru kwa kutoa mchango wangu huu, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Shangazi jiandae Mheshimiwa Leika.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi. Kwanza nimpongeze Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kutuletea Muswada huu ambao madhumuni yake ameyaeleza

lakini pia kwenye Hotuba ya Kamati pia tumeeleza madhumuni ya mabadiliko haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mabadiliko haya ya Sheria Mbalimbali Namba Tatu wa Mwaka 2023 yanalenga kwenda kuleta ufanisi katika Wizara mpya ya Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji. Kwa sababu tangu Mheshimiwa Rais ameunda Wizara hii maana yake Waziri mwenye dhamana tumemfunga mikono, hawezi kufanya kazi kwa sababu hati idhini ambazo zinamruhusu kufanya kazi kwenye Wizara hii ziko katika Wizara ya Viwanda na Biashara. Mabadiliko haya yanalenga kuleta ufanisi lakini kuifanya sasa Wizara mpya hii ikafanye kazi hasa kwa kupitia mabadiliko katika Sheria Namba 373 ambayo ni *The Export Processing Zone* kwa maana ya Kanda Maalum za Uwekezaji kwa Ajili ya Mauzo Nje ya Nchi (*Special Ecnomic Zone).*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili ni muhimu sana kwa sababu ndilo ambalo linaipa uhalali Wizara hii kufanya kazi. Sasa kama tusipofanya marekebisho haya maana yake Wizara itakuwa bado haijaanza kutekeleza wajibu wake ambao ndio umefanya iundwe. Lakini pamoja na sababu hizo sisi kwenye Kamati tumejadili kwa kina tumeridhika na madhumuni ya mabadiliko haya na kimsingi tumeunga mkono. Hata hivyo tunashauri baadhi ya mambo kadhaa ikiwemo eneo la kwanza ambalo tunapenda kushauri ni kwenye Ibara ya 14 ya Sheria hii ya *Export Processing Zone,* kanda maalum hii ya kiuchumi. Kwenye Ibara ya 14(1) imetaja muundo wa Bodi ya *EPZA*. Kwenye muundo huu wa bodi Mtendaji Mkuu wa Bodi ndiye anakua Katibu wa Bodi, na huko nyuma Waziri ndio alikuwa Mwenyekiti wa Bodi. Lakini kwenye *composition* kwenye muundo huu wako Makatibu kadhaa wanaingia kwa nafasi zao katika Bodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, yupo Katibu Mkuu anayehusika na Wizara ya Fedha, Katibu Mkuu Waziri ya Maji, Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, wote ni Wajumbe kwenye Bodi hii, lakini kwenye mabadiliko bado hawajaleta. Tunatamani kuona kwamba na Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji naye aingie kwenye Bodi kwa sababu Makatibu wenzake wote wanakuwa ni

Wajumbe wa Bodi, kwa hiyo ni vizuri na yeye akawepo hapo kwenye Bodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo tungependa kuipongeza Serikali ni hii dhana nzima ya kuitoa sasa kwenda kuondoa hiki Kifungu cha 4, kuondoa neno *"Minister responsible for industries"*. Kwa maana kwamba kwa kuliondoa hili neno linafanya sasa kwamba wakati wowote Mheshimiwa Rais anapoweza kutoa hati idhini kwenda Wizara yoyote, anaweza akahamisha majukumu ya *Special Economic Zone* ama *Export Processing Zone* kwenda mahali popote bila kuleta mabadiliko ya sheria. Kwa sababu tayari eneo hili limefanyiwa marekebisho ya jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Edward Olelekaita, jiandae *Attorney General*.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi na nimpongeze *Attorney General* kwa kuleta Muswada huu ambao lengo lake ni kubadilisha sheria mbili. Sheria ya Kanda Maalum ya Uwekezaji kwa ajili ya mauzo ya nje, Sura ya 373 na Sheria ya Kanda Maalum ya Kiuchumi, Sura 420.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge litakumbuka na niwapongeze Wanakamati wenzangu ambao wamechangia. Mtakumbuka kwamba Bunge hili lilipitisha sheria mpya kabisa baada ya mjadala mkubwa wa Wabunge kutaka tulete Tume mpya ya Mipango ya Nchi. Mtakumbuka Mwezi Juni, tulitunga sheria mpya na kwenye Sheria ile ya Mipango Kifungu cha 3 kinasema: *"Tume itaundwa na Mheshimiwa Rais na itakuwa na wajumbe wafuatao; moja, ni Waziri mwenye dhamana ya masuala ya mipango na maendeleo ya Taifa"*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo baada ya Bunge kupitisha Sheria hii ya Tume ya Mipango, tayari kabisa tulijua kwamba kuna

mabadiliko ya Serikali na tutakumbuka Mheshimiwa Rais tarehe 22 Juni, kupitia Gazeti la Serikali namba 407(b), Mheshimiwa Rais aliunda Wizara mpya ya Uwekezaji, Ofisi ya Rais, Uwekezaji na Mipango ambayo Mheshimiwa Profesa Kitila aliteuliwa kuwa Waziri wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mabadiliko hayo ni *process*, Bunge kwa sababu ya kuwa na Wizara mpya ilibidi na sisi tubadilishe Kanuni za Bunge kupitia Kamati ya Bunge ya Kanuni kubadilisha Nyongeza ya Nane ili kupanga Wizara pale kwenye Kamati na Majukumu ya Kamati na Wizara zinazokwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hata Bunge, sisi kupitia Kamati yetu tulibadilisha Kanuni za Bunge, Nyongeza ya Nane ambayo Bunge hili lilikasimu madaraka hayo kwa Kamati ya Kanuni ya Bunge. Kwa hiyo, baada ya *process* hiyo nyingine ya pili sasa, Mheshimiwa *Attorney General* ameleta sasa mabadiliko ya Sheria hizi mbili, *the Export Processing Zone Act* ili ku-*realign* shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo mabadiliko haya ni madogo sana na haya-*create* nanii yoyote, ni *definition* tu ya *Minister* kutoka *Minister responsible for Industries* iende kwa Minister ambaye atakuwa *responsible* kwa mambo ya uwekezaji. Nimshukuru Mheshimiwa *AG* kwa sababu ni kama ameongeza *innovation* kubwa hapa kwa kutokum-*define* tena Waziri kwa cheo chake na kusema tu Waziri atakayehusika na mambo ya *economic processing zone*. Maana yake, *logic* yake ni kwamba ikitokea mabadiliko mengine ya *realignment,* basi huyo huyo Waziri atakayechaguliwa, ambaye atakuwa anasimimamia masuala ya *export processing zones* tayari kwenye *instrument* yake itakuwa inataja tu bila kueleta mabadiliko mengine ya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, *so this is an innovation*, Mheshimiwa *Attorney General, big up*. Kwa hiyo, mtaona kama mabadiliko madogo haya ni kuwezesha tu *realignmen*t ya Serikali ili *functioning* ya Serikali iweze kwenda bila ku-*create lacuna*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya *processes* zote hizo za kuanzia Sheria ya Tume ya Mipango na Uwekezaji, baada ya Waziri kuteuliwa na baada ya Kanuni za Bunge kubadilishwa kwa maana ya ku-*realign,* Kamati na Wizara na sasa tunahitimisha kwa kuleta mabadiliko haya sasa ya sheria ambayo itampa Profesa Kitila kazi ya kwenda kufanya *field* sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati iliona labda huko mbele na tulimwambia Mheshimiwa *Attorney General* kwa sababu ya sheria hii ambayo wana-*amend* ile *composition* ya wale watu wa Kamati, sisi tuliona huko mbele wakiona haita-*create confusion* si mbaya kama Katibu Mkuu wa Wizara hii mpya sasa atakuwa sehemu ya Kamati hiyo kwa ajili ya *records*. *Of course*, tunafahamu na tunajua *logic* kwa nini hata ile sheria ambayo tunabadilisha sasa, Katibu Mkuu wa hiyo Wizara hakuwepo, kwa sababu Katibu wa Bodi hii ni *Director General* anayehusika na mambo ya *economic processing zones*, kwa hiyo hakuna *confusion* yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu mabadiliko haya ni madogo sana na nahitimisha kwa kifupi namna hiyo, naomba niwashawishi Wabunge tupitishe huu Muswada haraka sana ili wakaufanye kazi haraka sana. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Profesa Mkumbo, Waziri Ofisi ya Rais, Uwekezaji.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hoja. Naomba nitoe ufafanuzi wa jambo moja tu kuhusu *composition* ya Bodi ya *EPZA* kwa nini Katibu Mkuu asiwepo.

Kwanza dhana ya wale Makatibu Wakuu wawili kuwepo ni kwa sababu Bodi ya *EPZA* pamoja na mambo mengine inafanya uamuzi wa uwekezaji katika eneo husika. Kwa hiyo, tukishafanya uamuzi wa kujenga *industrial park,* kazi ya Serikali kubwa ni

kuwezesha ujenzi wa miundombinu husika; kama nishati, maji, barabara na kadhalika. Ilionekana kwamba wawepo ili uamuzi ukishafanyika, wahusika wa miundombinu ile wawe tayari ni sehemu ya uamuzi ili waweze kuharakisha utekelezaji wake. Kwa hiyo, ndio ni sababu ya msingi kwa nini wale Makatibu Wakuu wawili unaona wapo pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa nini Katibu Mkuu husika hayupo ni kwa sababu Waziri wa Sekta husika ndio Mwenyekiti, kwa hivyo kawaida unapomwona Waziri kimsingi unamwona Katibu Mkuu kwa sababu anayemwandaa Waziri ni Katibu Mkuu. Kwa hiyo kimsingi Katibu Mkuu wa Sekta husika yupo na kawaida huwa anahudhuria vikao. Sio mjumbe lakini Katibu Mkuu huwa anahudhuria kama *Ex- Officio*. Kwa hiyo, nadhani hilo halina ugumu na kama alivyosema Mheshimiwa Olelekaita, Mtendaji Mkuu wa *EPZA* kimsingi anafanya kazi chini ya usimamizi wa Katibu Mkuu. Kwa hivyo kimsingi Katibu Mkuu yupo pamoja na kwamba haonekani kwenye orodha ya Wajumbe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nilitaka nitoe ufafanuzi huo mdogo katika kuboresha hoja hii. Nakushuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante na hayo mabodi msiwe na urasimu mwingi, mnapoteza muda mwingi kujadili, jadili, jadili, *make decisions fast*, nchi iende. *(Makofi)*

Mheshimiwa *Attorney General.*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nasimama mbele yako na Bunge hili Tukufu kwa mara nyingine nikishukuru sana, napenda nitambue na kuheshimu sana michango ambayo Waheshimiwa Wabunge wamewasilisha hapa wakiongozwa na Makamu Mwenyekiti wa Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi yalioelezwa na kuchangiwa na Waheshimiwa Wabunge ambao wamepata fursa ya kutoa mawazo yao ndio uwasilishaji halisi wa maana ya uharaka na

mahitaji ya Muswada tuliowasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu. Kwa sababu kwa upande wetu Serikali bila kuwasilisha Muswada huu ni kweli wote tunajua kwamba sasa tupo Mwezi wa Tisa, *quarter* ya kwanza (robo ya kwanza) ya mwaka wa fedha imekwishamalizika lakini kwa Taasisi kama *EPZA* wameshindwa kufanya kikao cha Bodi hata kimoja kwa sababu ya hayo marekebisho ambayo tumewasilisha leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kwa hayo yote ambayo yamejadiliwa na maudhui ya Muswada huu, kingine ambacho niombe tu kuwaeleza Waheshimiwa Wabunge ni kwamba, kwa kuenzi maboresho makubwa ambayo Serikali inayafanya kwa maelekezo fasaha ya Mheshimiwa Rais, wote tunajua baada ya kuwepo kwa *Plan Commission,* kwa sasa kazi kubwa ya Serikali ni kuhakikisha kwamba ile Tume ya Mipango inaleta tija ambayo inategemewa kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa haya mawazo ambayo kwa nini Katibu Mkuu hayumo, nafikiri Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo ametoa ufafanuzi. Pia, niwahakikishie tu hawa Waheshimiwa Wabunge ambao wamepata fursa ya kuongelea jambo hilo niwaeleze tu kwamba, safari tuliyonayo ni ndefu. Baada ya *TIC* kuhamishiwa Ofisi ya Rais, Uwekezaji; baada ya *TR* kuhamishiwa Ofisi ya Rais, Uwekezaji, kwa hiyo sasa na hizi *EPZA* na mambo yote ambayo yatawezesha *Plan Commission*, kwa sasa *composition* ilivyo, wote tunajua kabisa yupo yule Mtendaji Mkuu wa Tume ya Mipango kama mmoja wa Wajumbe kwenye Tume hii, ambaye yeye kwa vyovyote uhusika wake ni wa maeneo yote na kuhakikisha kwamba inawezeshwa ile Tume na Wizara husika kutekeleza yale na Waziri mwenye dhamana sasa kuwajibika ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo maboresho yoyote ambayo yataendelea kuwasilishwa katika Bunge hili tukufu, naamini yataendelea kujenga zaidi mifumo yetu ya kuhakikisha kwamba suala la uwekezaji nchini linawekewa misingi imara ya kisheria, lakini ya kitaasisi na mazingira rafiki zaidi ya kuhakikisha kwamba Tume

hiyo na Wizara iliyopewa dhamana inaleta mabadiliko makubwa tofauti na ambavyo kulikuwa na changamoto zilizokuwa zinakwamisha hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa Bunge lako lifikirie haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na taadhima naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, hoja imeungwa mkono.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.3) wa Mwaka 2023 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Bill*, 2023]**

**MWENYEKITI:** Tukae.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2
Kifungu cha 3
Kifungu cha 4
Kifungu cha 5

Kifungu cha 6
Kifungu cha 7

*(Vifungu viliyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Mtoa Hoja.

**T A A R I F A**

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 102 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2023, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.3) wa Mwaka 2023 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.3) Bill, 2023)* Ibara kwa Ibara na kuukubali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.3) wa Mwaka 2023 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Bill, 2023)* sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, hoja hiyo imeungwa mkono. Sasa nitawahoji, kwamba sasa Bunge sasa likubali na kupitisha Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.3) wa Mwaka 2023 (*The Written Laws, Miscellaneous Amendments, (No.3) Bill, 2023)*.

Katibu.

**NDG. PILI OMARI – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali zipatazo mbili kwa lengo la kuondoa mapungufu ambayo yamejitokeza wakati wa utekelezaji wa baadhi ya masharti katika sheria hizo *(A Bill for an Act to Amend Certain Written Laws in order to keep the Laws Updated with some challenges observed in its implementation)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa nilikuwa sijawahoji. Nitarudia, kuwa Bunge sasa likubali Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.3) wa Mwaka 2023 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.3) Bill, 2023)*.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Katibu.

**NDG. PILI OMARI – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali zipatazo mbili kwa lengo la kuondoa mapungufu ambayo yamejitokeza wakati wa utekelezaji wa baadhi ya masharti katika sheria hizo *(A Bill for an Act to Amend Certain Written Laws in order to keep the Laws Updated with some challenges observed in its implementation)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

*(Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.3) wa Mwaka 2023 (The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.3) Bill, 2023) Ulipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kwa hatua hii sasa Bunge limekamilisha kazi yake na sasa niwapongeze Waheshimiwa wote; Mheshimiwa *AG*, Kamati kwa kweli mmefanya kazi nzuri sana. Haya ni mabadiliko makubwa yatakayoweza sasa kutoa fursa kwa utendaji na uboreshaji wa shughuli zilizoletwa leo zifanye vizuri kwenye Ofisi ya Rais na hasa kwenye uwekezaji. Uwekezaji ndio *engine* ya nchi kwenda mbele, kwa hiyo nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa *AG* na Mheshimiwa Waziri pamoja na Makatibu wetu.

Baada ya maneno hayo sasa, hatua hii sasa Muswada huu unakwenda kwa Mheshimiwa Rais, sisi tumemaliza kazi yetu. Hivyo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 6.23 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 7 Septemba, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*